



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

---

SHERIA YA MTOTO  
[SURA YA 13]

TAFSIRI YA KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO ZA MWAKA 2012

Toleo hili la Kanuni za Makao ya Watoto za mwaka 2012, Tangazo la Serikali Na. 155 la tarehe 4, mwaka 2012, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam  
28 April, 2016

GEORGE M. MASAJU,  
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

*Kanuni za Makao ya Watoto*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 166 la tarehe 13/05/2016

SHERIA YA MTOTO,  
(SURA YA 13)

---

**KANUNI**

---

*(Zimetungwa vifungu vyataga 145 na 175)*

---

**KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO  
MPANGILIO WA KANUNI**

*Kanuni kifungu*

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI**

1. Jina.
2. Tafsiri.

**SEHEMU YA PILI  
MISINGI YA JUMLA**

3. Misingi ya jumla.
4. Haki za watoto.

**SEHEMU YA TATU  
LESENI YA MAKAO YA KULELEA WATOTO**

5. Maombi ya leseni.
6. Usajili wa makao ya watoto.
7. Mahitaji kwa ajili ya kuanzisha na kusimamia makao ya watoto.

**SEHEMU YA NNE  
USIMAMIZI WA MAKAO YA KULELEA WATOTO**

8. Kamati za Ustawi wa Jamii.

9. Ushiriki wa mtoto.
10. Mahitaji ya wafanyakazi na ajira ya wafanyakazi.
11. Kanuni za maadili.
12. Kanuni za ulinzi wa mtoto.
13. Taratibu za kumtunza mtoto.
14. Wajibu wa kutunza kumbukumbu .
15. Taarifa za fedha na takwimu .

**SEHEMU YA TANO**  
**USAJILI, MPANGO WA MALEZI, MATIBABU NA MALEZI**

16. Usajili na mpango wa malezi.
17. Chakula na lishe.
18. Huduma za matibabu.
19. Malazi na vifaa vingine.
20. Elimu na mafunzo ya vitendo.

**SEHEMU YA SITA**  
**UUNGANISHAJI NA UONDOAJI**

21. Ziara na mawasiliano.
22. Maandalizi ya kuwaunganisha na kuwatoa watoto.
23. Kutolewa.

**SEHEMU YA SABA**  
**USIMAMIZI WA TABIA ZA MOTO**

24. Usimazi wa tabia.
25. Hatua za kinidhamu.
26. Uzuiaji wa matumizi ya nguvu.

**SEHEMU YA NANE**  
**UFUATILIAJI, UKAGUZI NA MALALAMIKO**

27. Ufuatiliaji na ukaguzi.
28. Ukaguzi wa makao ya watoto baada ya kupata malalamiko.
29. Miongozo ya Malalamiko.
30. Haki ya kulalamika.
31. Kumbukumbu ya malalamiko.
32. Daftari la malalamiko.

**SEHEMU YA TISA  
MASHARTI YA JUMLA**

33. Taarifa ya kifo.
34. Taratibu mbadala kwa mtoto baada ya kufutwa kwa leseni.
35. Masharti ya mpito.
36. Mamlaka kutengeneza fomu na taratibu.

SHERIA YA MTOTO  
(SURA YA 13)

---

**KANUNI**

---

*(Kifungu cha 145 na 175)*

---

**KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO**

**SEHEMU YA KWANZA**  
**MASHARTI YA UTANGULIZI**

Jina                   **1.** Kanuni hizi zitaitwa kama Kanuni za Makao ya Watoto za mwaka, 2012.

Tafsiri               **2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-  
Sura ya 13           “Sheria” maana yake Sheria ya Mtoto;  
                        “mlezi” maana yake ni mtu mwenye uzoefu wa miaka miwili na kuendelea aliyeajiriwa na makao ya watoto kutoa huduma ya malezi kwa watoto katika taasisi;  
                        “mfanyakazi wa malezi” maana yake ni mlezi au mfanyakazi wa kulea mtoto;  
                        “mlezi wa mtoto” maana yake ni mtu yejote mwenye cheti katika huduma za ustawi wa jamii cha kulea mtoto kutoka katika taasisi inayotambulika aliyeajiriwa na makao ya watoto kwa ajili ya kutoa malezi ya karibu, usimamizi na uangalizi wa watoto katika taasisi;  
                        “makao ya watoto” maana yake ni taasisi tofauti na shule iliyothibitishwa na mahabusu ya watoto ambapo watoto watano au zaidi wenye mazingira magumu au wenye mahitaji ya uanglizi au ulinzi hypolekewa, kulelewa na kutunzwa ama kwa hisani au kwa malipo na mtu asieme ndugu au mlezi wa mtoto;  
                        “ulinzi wa mtoto” maana yake ni kitendo kinachokusudia kuzuia na kutoa mwitikio kwa unyanyasaji, ukatili, uonevu na

utelekezaji wa mtoto;  
“Kamishna” maana yake ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii;  
“Idara” maana yake ni Idara ya Ustawi wa Jamii;  
“mtu mwenye ulemavu” maana yake ni mtu ambaye ana mapungufu ya mwili au akili ambayo yana madhara makubwa na ya muda mrefu kwa uwezo wa mtu huyo kutekeleza shughuli zake za kila siku;  
“Afisa Afya” maana yake ni Afisa afya katika utumishi wa umma au taasisi ya afya iliyopewa leseni;  
“taasisi” ina maana sawa na ile iliyotolewa kwake na Sheria na hajiumushi shule ya maadilisho, mahabusi za watoto na vituo nya dharura;  
“malezi ya kitaasisi” maana yake ni muungano wa taasisi na huduma zinazohudumia watoto wenyе mazingira hatarishi na watoto wenyе uhitaji wa malezi na ulinzi kwa ushirikiano;  
“leseni” maana yake leseni iliyotolewa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuendesha makao ya watoto;  
“mwenye leseni” maana yake ni mtu au taasisi iliyopewa leseni inayoiwezesha kuendesha makao ya watoto;  
Sura ya 287 na 288 “mamlaka ya serikali za mitaa” ina maana sawa na ile iliyotolewa kwake na Sheria za Mamlaka ya Serikali za Mtaa;  
“mtoto aliye katika mazingira hatarishi zaidi” maana yake ni mtoto mwenye uhitaji wa malezi na ulinzi kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 16 cha Sheria ya Mtoto anayekinzana au aliye na hatari ya kukinzana na sheria na mtoto mwenye ulemavu;  
“muda wa usiku” maana yake ni muda kati ya saa 4 usiku mpaka saa 12 alfajiri;  
“yatima” maana yake ni mtoto mwenye umri chini ya miaka 18 aliyefiwa na mzazi mmoja au wote wawili;  
“afisa ustawi wa makao” maana yake ni mtu mwenye stashahada ya juu katika huduma za jamii au shahada ya sosholojia, akiwa na uzoefu wa mwaka mmoja aliyeajiriwa na makao ya watoto kutelekeza majukumu ya siku kwa ajili ya malezi na ustawi wa watoto na usimamizi wa wafanyakazi wa walezi;  
“afisa wa ustawi wa jamii” maana yake ni Afisa wa ustawi wa jamii mwenye jukumu la kusimamia mamlaka mijini, manispaa, wilayani au halmashauri za jiji;

**SEHEMU YA PILI  
MISINGI YA JUMLA**

Misingi ya  
jumla

3. Pale ambapo mtoto ametenganishwa na mazingira ya familia yake, maamuzi juu ya uangalizi wake yatazingatia kanuni za jumla zifuatazo-
- (a) kwamba mtoto atakuzwa katika mazingira ya familia kwa ajili ya kulinda maendeleo yake na utu wake;
  - (b) kwamba matarajio na fikra za mtoto zitatambuliwa na zitazingatiwa kulingana na umri, maendeleo, na uelewa wa mtoto;
  - (c) kwamba kumweka mtoto katika makao ya watoto utakuwa ni hatua ya muda na si ya kudumu na lazima itumike pale ambapo hakuna njia nyingine ya kumsaidia mtoto;
  - (d) kwamba kumweka mtoto utazingatia zaidi misingi ya kifamilia kuliko misingi ya kitaasisi;
  - (e) kwamba kumweka mtoto utazingatia misingi ya kitaifa zaidi kuliko misingi ya kimataifa;
  - (f) kwamba maamuzi juu ya uwekaji wa mtoto utazingatia maslahi bora mtoto;
  - (g) kwamba kipaumbele kitatolewa kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na mwendelezo katika makazi ya mtoto, dini ya mtoto na chimbuko la utamaduni wake;
  - (h) kwamba vyombo vya umma vitaamua kwa wakati kuhusu masuala yanayohusu watoto;
  - (i) kwamba mtoto ye yeyote aliyewekwa kwenye makao ya watoto atakuwa na haki ya kupata cheti cha kuzaliwa, kwa mtoto ambaye hana cheti cha kuzaliwa, Meneja kwa haraka iwezekanavyo atatafuta cheti cha kuzaliwa na taasisi itagharimia mchakato huo;
  - (j) kwamba mtoto mwenye ulemavu atakuwa na haki ya kupewa malezi, huduma, nyenzo za kujimudu fursa sawa katika elimu na mafunzo pale itakavyowezekana kwa ajili ya kuendeleza kipaji na uwezo wake kwa kujitegemea; na
  - (k) kwamba watoto ndugu hawatatenganishwa

isipokuwa tu pale ambapo maslahi yao yanaelekeza hivyo.

Haki za watoto

**4.-**(1) Maslahi ya mtoto yatakuwa ni zingatio la msingi wakati wa kuchukua hatua au kufanya maamuzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Kila mtoto aliyepokelewa katika makao ya mtoto atakuwa na haki ya-

- (a) kuhudumiwa kwa heshima na bila kubaguliwa kwa aina yejote, ikijumuisha kwa misingi ya jinsia, rangi, dini, lugha, itikadi za kisiasa, ulemavu hali ya afya, mila, kabila, historia ya anakotoka, mahali alipozaliwa, hali ya uchumi, kwa kuwa mkimbizi au hadhi nyingine yoyote;
- (b) kupata malezi na msaada ambao utazingatia mahitaji yake binafsi kwa kuzingatia umri, jinsi, ulemavu, hali ya afya na mazingira binafsi ya mtoto;
- (c) kupata lishe ya kutosha, mavazi na malezi ya mtoto;
- (d) kupata huduma za matibabu ya aina zote mbili yaani ya kuzuia na kutibu;
- (e) elimu na mafunzo stahiki kwa kuzingatia umri, ukomavu na uwezo wake;
- (f) usiri, umiliki na ulinzi wa mali zake;
- (g) kujulishwa tabia inayotarajiwa kwake na madhara ya kutokuzingatia tabia hiyo;
- (h) kulindwa dhidi ya aina yejote ya ukatili, unyanyasajji, utelekezwaji na unyonywaji;
- (i) kutoteswa, unyanyaswaji au kutendewa vitendo vya ukatili, vitendo visivyo vya kibinadamu au kushusha hadhi au adhabu ikiwa ni pamoja na vitendo vya kitamaduni ambavyo vinashusha hadhi ya utu au vinamadhara dhidi ya ukuaji wa kimwili na kiakili;
- (j) kuwasiliana mara kwa mara na kutembelewa na wazazi, mlezi, wanafamilia, mshauri wa dini, wanataluma wa afya ya makazi, wanasaikologia, wawakilishi wa kisheria na mtu yejote muhimu katika maisha ya mtoto, isipokuwa kama kuna amri

- ya mahakama inayozuia au mtoto amechagua vinginevyo;
- (k) kupata muda wa kutosha kwa kila siku kwa ajili ya kupumzika, kufanya mazoezi na kucheza;
- (l) kulindwa dhidi ya ajira hatarishi na zenye madhara;
- (m) kushirikishwa na kutoa maoni yake kulingana na uwezo wake kuhusu maamuzi yenye athari kwake; na
- (n) kupata msaada unaohitajika na kupata mkalimani endapo lugha au ulemavu ni kikwazo ilikushauriana juu ya maamuzi ambayo yana athiri makazi au malezi na maendeleo yake.

#### SEHEMU YA TATU

##### LESENI YA MAKAO YA KULELEA WATOTO

Maombi ya  
leseni

**5.-**(1) Mtu yejote anayekusudia kuendesha makao ya watoto atatakiwa, kabla ya kuanza kuendesha makao hayo kuomba na kupata leseni kwa Kamishna.

(2) Maombi ya leseni chini ya kanuni ndogo ya (1) yatawasilishwa kwa utaratibu ulioainishwa katika Fomu Na.2(a) katika Jedwali endapo mwombaji ni mtu binafsi na kwa utaratibu ulioainishwa katika Fomu Na.2(b) endapo mwombaji ni taasisi.

(3) Mwombaji atawasilisha fomu iliyojazwa kwa afisa ustawi wa jamii wa jiji, manispaa, mji au halmashauri ya wilaya.

(4) Fomu ya muombaji inayotajwa katika kanuni ndogo ya (2) itaambatana na barua ya utambulisho kutoka kwa afisa mtendaji wa kata pamoja na nakala iliyoabitishwa ya cheti cha usajili endapo mwombaji ni taasisi.

(5) Afisa ustawi wa jamii atafanya uchunguzi wa kijamii wa maombi husika atafanya tathimini ya majengo, mwombaji na kwa madhumuni hayo uchunguzi utajumuisha kutembelea majengo yanayopendekezwa na kutathimini ubora wake kwa kuzingatia umri na aina ya watoto wanaokusudiwa kuishi katika nyumba hiyo, mkutano na mwombaji na mdhamini na mamlaka ya Serikali za mitaa kwa ajili ya kukusanya taarifa za mwombaji wa eneo hilo.

(6) Afisa afya wa jiji, manispaa, mji au halmashauri ya wilaya atafanya ukaguzi wa majengo na atamshauri muombaji

endapo kuna marekebisho yejote yanayotakiwa kufanywa kabla leseni haijaidhinishwa.

(7) Afisa afya wa jiji, manispaa, mji au halmashauri ya wilaya ataandika taarifa ya ukaguzi wa majengo ambayo itajumuisha mapendekezo endapo leseni itolewe, na atawasilisha taarifa hiyo kwa afisa ustawi jamii ndani ya siku thelathini tangu siku ya kupokea maombi.

(8) Afisa ustawi wa jamii wa jiji, manispaa, mji au halmashauri ya wilaya atawasilisha kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii ndani ya siku 60 tangu alipopokea maombi, fomu ya maombi na kutoa mapendekezo juu ya endapo leseni itolewe kwa kutumia fomu inayofanana na Fomu Na.2(c), sambamba na ripoti ya uchunguzi wa kijamii, muundo na usajili wa taasisi taarifa ya afya ya ukaguzi wa jengo, taarifa za uwezo wa juu wa makao ya watoto na orodha ya wafanyakazi wa makao ya watoto na nakala ya vyeti vyao.

(9) Kamishna atatoa mwongozo wa fomu juu ya utaratibu wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kufanya uchunguzi kwa mujibu wa kanuni hii.

Usajili wa  
makao ya  
watoto

**6.-**(1) Baada ya kupokea maombi, Kamishna wa Ustawi wa Jamii atayapitia maombi hayo ndani siku 30 tangu alipoyapokea maombi hayo na endapo maombi yatakuwa yamekidhi mahitaji muhimu, ataidhinisha maombi hayo kwa kujaza Fomu Na.2(c), na atatoa leseni kwa muombaji na kumtaarifu afisa ustawi wa jamii ndani ya siku 14 tangu siku ya uamuzi na atainingiza taarifa za makao ya kulelea watoto katika Rejista ya Makao ya Watoto kwa kutumia Fomu Na.1.

(2) Pale ambapo maombi hayakukidhi mahitaji ya Sheria na kanuni zake, Kamishna atakataa maombi kuititia Fomu Na.2(c), na atamtaarifu mwombaji kwa kuititia afisa ustawi wa jamii husika ndani ya siku 14 tangu siku ya uamuzi na sababu za kukataa.

(3) Leseni ya kuendesha makao ya kulelea watoto itatolewa kwa mwombaji katika Fomu Na.3.

(4) Leseni iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (3) haitahamishika kwenda kwa jengo, mtu au taasisi nyingine.

(5) Mwombaji ambaye hakuridhishwa na kukataliwa kwa maombi yake ya leseni atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa waziri anayehusika na masuala ya ustawi wa jamii ndani ya siku

thelathini tangu alipopokea taarifa ya kukataliwa na atapewa fursa ya kusikilizwa kabla waziri hajafanya maamuzi ya rufaa.

(6) Waziri atapitia rufaa ndani ya siku sitini tangu kupokelewa kwa rufaa na atatoa uamuzi wa rufaa hiyo.

(7) Uamuzi wa Waziri utakuwa wa mwisho.

(8) Mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa hatazuiliwa kuleta maombi mengine isipokuwa kipindi cha miezi kumi na mbili lazima kiwe kimepita tangu alipoleta maombi ya awali.

Mambo ya  
kuzingatia kwa  
ajili ya  
kuanzisha na  
kusimamia  
makao ya  
watoto

7. Ili leseni ya makao ya watoto iweze kutolewa, mwenye leseni lazima athibitishe-

- (a) uwepo wa majengo bora ambayo yanakidhi viwango vilivyoainishwa katika kanuni hizi;
- (b) uwepo wa hatimiliki ya jengo au mkataba wa pango unaota notisi ya angalau miezi sita endapo mkataba huo utavunjwa;
- (c) kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (4) na kanuni ya 35 ya kanuni hizi, idadi ya wafanyakazi watakaohitajika kukidhi viwango vilivyoainishwa katika kanuni ya 10 ya kanuni hizi; na
- (d) kwa makao mapya ya watoto, mwenye leseni atatakiwa ndani ya miezi sita tangu alipopata leseni kuwasilisha orodha ya wafanyakazi na sifa zao kwa afisa ustawi wa jamii na hataruhusiwa kupokea watoto katika makao ya watoto mpaka pale idadi ya wafanyakazi iliyoinishwa katika kanuni ya 10 itakapokuwa imetimia.

#### **SEHEMU YA NNE**

#### **USIMAMIZI WA MAKAO YA KULELEA WATOTO**

Kamati ya  
Ustawi wa  
Jamii

8.-(1) Itaanzishwa kwa kila makao ya watoto, kwa mujibu wa kifungu cha 134(2) cha Sheria, kamati ya ustawi wa jamii kwa ajili ya kusimamia uendeshaji na utawala wa ustawi na maendeleo ya watoto.

(2) Kamati ya ustawi wa jamii itaundwa na kuteuliwa chini ya kifungu cha 134(2) cha sheria kwa mujibu wa utaratibu ufuataao-

(a) mwenye leseni ya makao ya watoto baada ya

kushauriana na wajumbe watarajiwa juu ya utayari wao kuteuliwa kuwa wajumbe wa kamati, atawasilisha orodha ya majina kwa afisa ustawi wa jamii ambaye anaweza kuthibitisha orodha hiyo na kuwataarifu kwa maandishi juu ya uteuzi wao kuwa wajumbe wa kamati;

(b) katika kuchagua wajumbe wa kamati, mwenye leseni atawajumuisha wafuatao:

- (i) Afisa Afya wa kata ambaye atakuwa mjambe mwalikwa;
- (ii) Afisa Maendeleo wa kata ambaye atakuwa mjambe mwalikwa;
- (iii) Mwenyekiti wa Kijiji au mtaa ambaye atakuwa mjambe mwalikwa;
- (iv) wajumbe wawili kutoka katika eneo husika, mmoja kati yao atakuwa mwanamke;
- (v) wajumbe wawili kutoka kwenye Kamati ya Watoto waliokatika mazingira hatarishi zaidi, mmoja kati yao atakuwa mwanamke;

(c) Kamati ya Ustawi wa Jamii itateua Mwenyekiti wake;

(d) meneja wa makao ya watoto atakuwa katibu wa kamati ya ustawi wa jamii;

(e) kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2)(f), kamati za ustawi wa jamii zitadumu kwa kipindi cha miaka mitatu; na

(f) kwa ajili ya kuruhusu uongozi wa mpito, afisa ustawi wa jamii anaweza kuongeza kipindi cha ujumbe cha wajumbe wowote wawili atakaowateua kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

(3) Wajumbe wote watarajiwa wa Kamati watakaguliwa kabla ya kuteuliwa ili kujiridhisha kwamba hawana kumbukumbu zozote za zamani za makosa ya jinai na hasa kumbukumbu za makosa ya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya watoto na kwamba kila mmoja anafaa kufanya kazi na watoto.

(4) Kwa kuzingatia matakwa ya kanuni ndogo ya (8) ya kanuni hizi, Kamati ya Ustawi wa Jamii itajiwekea utaratibu wake wa utendaji.

(5) Kamati ya Ustawi wa Jamii itahakikisha kwamba makao ya watoto inakidhi ustawi wa watoto, ikiwa ni pamoja na

malezi, ulinzi, usimamizi afya, elimu, usalama kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na kanuni hizi.

(6) Ilukidhi malengo yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (5) hapo juu, Kamati ya Ustawi wa Jamii-

- (a) itakutana angalau mara nne kwa mwaka;
- (b) itatembelea eneo la makao na kufanya mazungumzo, wafanyakazi na watoto; na
- (c) itatoa mapendekezo kwa meneja na mwenye leseni.

(7) Ilukidhi malengo yaliyoinishwa kwenye kanuni ndogo ya (5), Kamati ya Ustawi wa Jamii itakuwa na mamlaka ya-

- (a) kuingia katika makao ya watoto muda wowote, kuzungumza na wafanyakazi wa makao ya watoto kwa lengo la kutekeleza mamlaka yake;
- (b) kukagua majalada au kumbukumbu za hesabu wakati wowote;
- (c) kumuamuru au kumuita meneja au mwenye leseni ya makao ya watoto kuja mbele ya Kamati kujibu maswali yeoyote;
- (d) kumshauri Kamishna juu ya masuala yanayohusu kazi zinazotakiwa kufanywa na mtoto katika taasisi; na
- (e) kujiridhisha juu ya huduma kwa watoto katika taasisi, hali ya jengo na utawala wa taasisi.

(8) Mwenye leseni na meneja watachukua hatua za kutekeleza mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii.

(9) Pale ambapo mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii anapata taarifa kuhusu malalamiko ya ulinzi wa mtoto atatoa taarifa na malalamiko hayo mara moja kwa afisa ustawi wa jamii.

(10) Kamati ya Ustawi wa Jamii itashauriana na watoto wanaoishi katika makao ya watoto mara kwa mara, na kwa malengo hayo-

- (a) watoto katika makao ya watoto watafahamishwa mara kwa mara kuhusu kazi ya kamati ya ustawi wa jamii na mwenyekiti au mjumbe aliyeandalialiwa;
- (b) watoto watawezeshwa na meneja kumchagua mwakilishi kutoka mionganini mwao kwa kila kipindi cha miezi sita, ambaye atawezeshwa ili kukusanya maoni ya watoto kuhusu matunzo na malezi;

- (c) mwakilishi wa watoto atakaribishwa kuwasilisha maoni ya watoto waliopo katika makao husika katika mukutano wa Kamati ya Ustawi wa Jamii angalau mara mbili kwa mwaka; na
- (d) Kamati ya Ustawi wa Jamii itachukua hatua muafaka kujibu hoja kwa wakati zilizotolewa na mwakilishi wa watoto na itamjulisha mwakilishi wa watoto ndani ya siku thelathini tangu siku ya mukutano juu ya hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa.

Ushiriki wa  
mtoto

**9.** Kila meneja wa makao ya watoto atachukua hatua za kuhakikisha kwamba watoto wote wenyewe uwezo wa kutoa maoni wanahusishwa katika maamuzi yanayohusu uendeshaji wa makao hasa maamuzi ambayo yanaathari ustawi wao.

Ikama na ajira  
ya wafanyakazi

**10.-(1)** Kila mwenye leseni ataajili idadi ya wafanyakazi wenyewe vigezo na waliofunzwa kwa kadiri watakavyohitajika katika kuendesha makao ya watoto, kwa kuzingatia idadi, usawa wa kijinsia, umri, hali ya afya na mahitaji ya watoto wanaoishi katika makao hayo.

(2) Mwenye leseni atahakikisha kwamba angalau wafanyakazi wafuatao wanaajiriwa-

- (a) meneja mmoja atakaye kuwa na wajibu wa kuendesha makao ya watoto kwa kila siku;
- (b) afisa ustawi wa jamii ambaye ataidhinishwa kuwa afisa mfawidhi mwenye wajibu wa shughuli za kila siku za malezi na ustawi wa watoto na mwenye wajibu wa kusimamia wafanyakazi na ambaye atakuwa na angalau stashahada ya juu ya ustawi wa jamii au shahada ya sosholojia mwenye usoefu wa kitaaluma wa mwaka mmoja unaohusiana moja kwa moja na kazi za jamii kwa watoto.

(3) Mwenye leseni atahakikisha kwamba wafanyakazi wa kutosha wanaajiriwa na kupewa mafunzo kwa ajili ya kutoa malezi na usimamizi kulingana na idadi ya watoto waliopo katika makao ya watoto ili kuhakikisha kwamba mfumo wa utendaji unatekelezwa, na ili kukidhi uwiano wa wafanyakazi waliopo kazini na watoto waliopo kama ilivyoainishwa katika kanuni ndogo ya (8), (9) na (10) na katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

- (4) Wafanyakazi wa malezi watajumuisha-
- (a) walezi wa watoto, ambao watatakiwa kuwa na angalau astashahada katika huduma za ustawi wa jamii au malezi ya watoto kutoka katika taasisi inayotambulika walioajiriwa kutoa huduma ya malezi ya karibu, usimamizi na miongozo kwa watoto katika makao ya kulelea watoto; na
  - (b) mlezi ni mtu ambaye atakuwa na angalau uzoefu wa mwaka mmoja au zaidi kwa watoto aliyeajiriwa na makao ya watoto kutoa huduma ya malezi ya kila siku kwa watoto katika taasisi.

(5) Mwenye leseni atahakikisha kwamba kuna usawa baina ya wanaume na wanawake kwa kuzingatia idadi ya wasichana na wavulana ambao wanatunzwa katika makao ya watoto.

(6) Kwa makao ya watoto ambayo wanatunza watoto wenye ulemavu, magonjwa sugu au watoto wenye virusi vya ukimwi, mbali na mahitaji yalioainishwa katika kanuni hii, mwenye leseni atahakikisha kwamba ana ajiri afisa tiba mwenye stashahada ya utabibu.

(7) Idadi ya wafanyakazi wa ziada ambayo itajumuisha wafanya usafi, wapishi, walinzi, na wafanyakazi nyingine wataajiriwa ili kuhakikisha kuwa makao ya watoto yanaendeshwa kwa kuzingatia ulinzi.

(8) Meneja atahakikisha kwamba uwiano ufuatao wa wafanyakazi walio zamu na watoto inazingatiwa:

- (a) wafanyakazi wa malezi/watoto waliopo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza, na bila kujali idadi ya watoto wanaotunzwa, angalau wafanyakazi wa malezi wa zamu kila wakati;
- (b) kutakuwa na mfanyakazi wa malezi ya mtoto mmoja wa zamu kwa kila wafanyakazi wa malezi wa zamu wa tano;
- (c) kutakuwa na afisa mfawidhi kila wakati, au kama hayupo naibu afisa mfawidhi ambaye atakuwa ni mfanyakazi mkazi endapo wameajiriwa zaidi ya mmoja au mfanyakazi wa malezi ya mtoto atakayepangwa na meneja;
- (d) mfanyakazi mmoja aliyefundishwa huduma ya kwanza kila wakati; na

(e) mfanyakazi mmoja aliyefundishwa namna yakutumia vifaa vya zimamoto kila wakati.

(9) Inapotokea kuwa makao ya watoto inatunza watoto zaidi ya hamsini, zaidi ya mahitaji yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2) na (8), wafanyakazi wakazi wawili wataajiriwa.

(10) Kwa makao ya watoto yanayohifadhi watoto wenye ulemavu, magonjwa sugu au watoto wanaoishi na maambukizi ya virusi vya ukimwi meneja atahakikisha kwamba kuna mfanyakazi mmoja wa zamu wa malezi kwa kila watoto watano.

(11) Mwenye leseni atahakikisha kwamba wafanyakazi wanaojihusisha na watoto ni wafanyakazi wasio na maambukizi ya virusi vya ukimwi.

(12) Mwenye leseni, kwa kusaidiwa na afisa ustawi jamii pamoja na polisi atawachunguza wafanyakazi watarajiwa kabla ya kuajiriwa ili kujiridhisha kwamba hawana kumbukumbu ya makosa ya jinai, ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na kila mmoja anafaa kwa kazi ya watoto.

(13) Mwenye leseni atahakikisha kwamba-

(a) wafanyakazi wote bila kujali nyadhifa zao, wanapewa mafunzo ya awali ambayo yatajumuisha mafunzo juu ya kanuni zinazosimamia makao ya watoto, kanuni za maadili na sera na taratibu zinazosimamia ulinzi wa watoto; na

(b) mafunzo katika kazi ya mara kwa mara ambayo ni muafaka kwa kila wadhifa yanatolewa kwa wafanyakazi ili kuwawezesha kufanya kazi ipasavyo katika makao ya watoto, na hii itajumuisha-

(i) kumuendezea mtoto na msaada wa kisiakolojia;

(ii) mbinu za kurekebisha tabia;

(iii) masuala ya kijinsia;

(iv) masuala ya ulinzi wa watoto ikiwa ni pamoja na taratibu za kumlinda mtoto na maadili; na

(v) utunzaji wa kumbukumbu na usimamizi wa mashauri.

Kanuni za  
maadili

**11.** Wafanyakazi wote wa makao ya watoto, wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, wawakilishi nje ya wakala au idara, taasisi binafsi ikijumuisha mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za kidini, watu wanaojitolea wanaotembelea makao ya

watoto watatakiwa angalau kuweka saini na kufuata maadili yaliyoainishwa katika Jedwali la Pili la kanuni hizi ambayo itarekebishwa mara kwa mara na kutangazwa na Waziri katika Gazeti la Serikali.

Kanuni za ulinzi  
wa mtoto

**12. Ulinzi wa mtoto utazingatia kanuni zifuatazo-**

- (a) watoto wote bila kujali jinsia, umri, rangi, dini, lugha, mlengo wa kisiasa, ulemavu, hali ya afya, utamaduni, ukabila, kijiji au mji atokako, kuzaliwa, hali ya uchumi wa kijamii, kuwa mkimbizi au wa hadhi yoyote atakuwa na haki ya kulindwa dhidi ya majeraha, kutelekezwa, kunyanyaswa kijinsia, kunyonywa kijinsia na namna ye yeyote ya unyanyasaji na itakuwa ni wajibu kwa kila mfanyakazi kuhakikisha kwamba watoto wanalindwa;
- (b) maslahi bora ya mtoto yatapewa kipaumbele;
- (c) madai na tuhuma za ukiukwaji wa maadili ya ulinzi wa mtoto yatapewa uzito na yatashughulikiwa kwa wakati na kwa namna muafaka;
- (d) ukatili, unyanyasaji, unyonyaji, na utelekezaji wa mtoto vitachukuliwa kuwa ni vitendo vya ukiukwaji mkubwa na vitachukuliwa kuwa ni sababu za msingi za kuchukuliwa hatua za nidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi; na
- (e) hakuna mtoto atakaye adhibiwa au kwa namna ye yeyote ile kuonewa kwa sababu ya kuleta tuhuma za ukatili, unyanyasaji, unyonyaji au kutelekezwa.

Taratibu za  
kumtunza mtoto

**13.-(1)** Mwenye leseni ya makao ya watoto atahakikisha kwamba kuna taratibu za kuwatanza watoto ambazo zitaainisha namna gani tuhuma na ufichuaji wa malalamiko kuhusu ulinzi wa mtoto vitakavyoshughulikiwa na taasisi.

(2) Utaratibu wa ulinzi wa mtoto utaainisha angalau viwango vifuatavyo-

- (a) uchunguzi wa awali kufanya ndani ya masaa 24;
- (b) mtoto anajulishwa taratibu zote na anakuwa na haki ya kushiriki na kutoa maoni yake;
- (c) mtoto anapata misaada na usaidizi wote muhimu ikiwa ni pamoja na matibabu, ushauri na kujengewa imani.

- (3)(a) Haki ya faragha na utu wa mtoto inalindwa;
- (b) hatua za haraka zinachukuliwa kuhakikisha usalama wa mtoto unakuwepo ikiwa ni pamoja, na, pale itakapohitajika, kumsimamisha kwa muda mfanyakazi yejote ambaye tuhuma zinaelekezwa dhidi yake na kumzuia asiingie kwenye majengo ya makao ya watoto na kufanya mawasiliano yejote na mtoto aliyetoa tuhuma au mtoto mwininge yejote anayeishi katika makao hayo wakati uchunguzi wa tuhuma ukiwa unaendelea;
- (c) mfanyakazi anayetuhumiwa anajulishwa kuhusu maendeleo ya uchunguzi;
- (d) mashtaka ya nidhamu au jinai yanafunguliwa pale itakapofaa;
- (e) mwenye leseni anajulishwa mara moja juu ya tuhuma; na
- (f) hatua zote zinazochukuliwa zinazingatia maslahi mapana ya mtoto kama kipaumbele.

(4) Katika malalamiko yoyote kuhusiana na tuhuma za ukatili, unyanyasaji au unyonyaji wa mtoto, taratibu za ulinzi wa mtoto zitazingatiwa bila kujali taratibu za malalamiko zilizoainishwa katika Sehemu ya Nane ya Kanuni hizi.

(5) Mwenye leseni atahakikisha kwamba kanuni za utaratibu wa ulinzi za maandishi zinakuwepo kwa ajili ya wafanyakazi, watoto, wazazi, walezi na wageni na kwamba watoto wanajulishwa juu ya uwepo wa kanuni za taratibu hizo wakati wanaingia kwenye makao ya watoto katika utaratibu unaoleweka.

Wajibu wa  
kutunza  
kumbukumbu

**14.-(1)** Kila mwenye leseni ya makao ya mtoto atahakikisha kwamba anatunza rejestra ambayo itakuwa na kumbukumbu sahihi na zinazoenda na wakati kuhusu watoto wanaotunzwa katika taasisi hiyo kama vile umri, majina, majina ya kuzaliwa, historia ya dini, anuani ya mwisho ya wazazi inayojulikana, jinsia, maelezo kuhusu ndugu yejote na ulemavu wowote unaojulikana.

(2) Mwenye leseni, pamoja na yaliyoelezwa hapo juu, atahakikisha rejestra zifuatazo zinakuwepo-

- (a) rejestra ya kuwapokea na kuwaondoa watoto makaoni;

- (b) rejesta ya ajali ambamo tukio lolote muhimu linalohusu makao ya watoto litaingizwa;
- (c) rejesta ya wageni ambamo taarifa za wageni wote katika makao ya watoto zitaingizwa;
- (d) rejesta ya udhibiti wa tabia za watoto ambamo hatua za nidhamu zilizochukuliwa dhidi ya mtoto kwa mujibu wa kanuni hizi zitaingizwa;
- (e) rejesta ya malalamiko ambamo malalamiko yote chini ya kanuni hizi na ufumbuzi wake yataingizwa;
- (f) majalada ya kesi kwa kila mtoto ambayo yatajumuisha-
  - (i) fomu ya kupokelewa;
  - (ii) mpango wa malezi kwa ajili ya mtoto;
  - (iii) taarifa ya maendeleo ya mtoto;
  - (iv) mpango wa mtangamao;
  - (v) kumbukumbu za uchunguzi wa kitabibu na matibabu;
  - (vi) kumbukumbu za elimu kwa kila mtoto; na
  - (vii) kumbukumbu za familia, ikiwa ni pamoja na taarifa za mawasiliano wakati wa dharura.

Taarifa za fedha  
na takwimu

**15.-**(1) Kila mwenye leseni-

- (a) ataweka pamoja taarifa za mwezi na mwaka kuhusu watoto waliopo, waliosajiliwa na walioondolewa kutoka kwenye makao ya watoto na sababu za kusajiliwa na kuondolewa katika kipindi hicho na taarifa hizi zitakuwa kwenye Fomu Na.10 na Fomu Na.11 kwa kufuatana na zitawasilishwa kwa Afisa Ustawi wa Jamii; na

- (b) atawasilisha taarifa ya mwaka ya fedha kwa Afisa Ustawi wa Jamii katika Fomu Na.4 katika kipindi cha mwezi mmoja wa mwisho wa mwaka.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii kuwasilisha kumbukumbu hizi kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

(3) Kamishna atatoa muongozo wa ziada na namna ya ukusanyaji wa uwasilishaji wa kumbukumbu za makao ya watoto kwa Afisa Ustawi wa Jamii na Idara.

**SEHEMU YA TANO**  
**USAJILI, MPANGO WA MALEZI, MATIBABU NA MALEZI**

Usajili na  
mpango wa  
malezi

**16.-**(1) Hakuna mtoto atakayepokelewa katika makao yoyote ya watoto bila ridhaa ya mzazi, wazazi, ndugu au mlezi kwa kadri itakavyokuwa isipokuwa pale ambapo Afisa wa ustawi wa jamii amemwingiza mtoto kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria kwa amri ya malezi au malezi ya muda kwa mujibu wa kifungu cha 137(1) cha Sheria, ambapo katika mazingira hayo Afisa wa Ustawi wa Jamii ndiye atakayetoa ridhaa.

(2) Ridhaa inayohitajika chini ya kanuni ndogo (1), itakuwa katika Fomu Na.5.

(3) Meneja au Afisa Mfawidhi atahakikisha kwamba watoto waliosajiliwa chini ya mazingira yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) na (4) wanaoingizwa kwenye Rejesta ya kuwapokea na kuwaondoa makaoni.

(4) Mahitaji ya kanuni ndogo ya (1) na (2) hayatatumika katika hali ya dharura ambapo-

- (a) mtoto amekuja mwenyewe kwenye makao; au
- (b) pale ambapo mtu ambaye si mzazi au mlezi anapomleta mtoto katika makao ya watoto.

(5) Iwapo mtoto amesajiliwa katika mazingira yaliyoainishwa katika kanuni ndogo (4), meneja wa makao ya kulelea watoto atamjulisha Afisa ustawi wa jamii mapema iwezekanavyo, lakini kwa namna ye yeyote ile katika muda usiozidi masaa 48, kuanzia muda ambaa mtoto amepokelewa kwa muda.

(6) Pale ambapo mtoto amepokelewa kwa mujibu wa kanuni ndogo (3), Afisa Ustawi wa Jamii atafanya uchunguzi wa kijamii ndani ya siku 7, na atajaza fomu inayofanana na Fomu Na.6, na kama mtoto hawezi kurudishwa nyumbani mara moja, atatoa mapendekezo chini ya kifungu cha 137(b) cha sheria au idhini chini ya kifungu cha 137(c) cha sheria kwamba mtoto amepokelewa rasmi kwenye makao ya watoto.

(7) Baada ya kupokelewa rasmi kwenye makao ya kulelea watoto, meneja atahakikisha kwamba kumbukumbu za usajili zimejazwa katika Fomu Na.7 na zimewekwa kwenye jalada binafsi la mtoto.

(8) Ndani ya wiki moja baada ya mtoto kupokelewa katika makao ya mtoto, afisa ustawi wa makao atafanya tathimini ya hali ya kisaikolojia, kiafya, kielimu, maendeleo na mahitaji

mengine, na kwa madhumuni haya atatoa taarifa ya uchunguzi wa kijamii iliyoandaliwa na Afisa Ustawi wa Jamii na taarifa ya afya iliyoandaliwa na Afisa Afya.

(9) Kwa kuzingatia tathimini iliyofanywa chini ya kanuni ndogo (8), afisa ustawi wa makao ataandaa mpango wa malezi ambao utaainisha utaratibu wa namna makao ya mtoto itakavyokidhi mahitaji ya mtoto, kwa kushauriana na Afisa Ustawi wa Jamii, mtoto, endapo ana uwezo wa kutoa maoni yake, na, pale inapofaa wazazi au walezi wa mtoto.

(10) Afisa ustawi wa makao atafanya kazi na wafanyakazi wa malezi na wataalam wengine muhimu kutekeleza mpango wa malezi na mara kwa mara ataufanya mapitio mpango huo kuhakikisha kwamba unakidhi mahitaji ya watoto.

(11) Kamishna atatoa miongozo ya uandaaji wa muongozo wa malezi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (10).

Chakula na lishe

**17.-**(1) Kila mwenye leseni atahakikisha kwamba kila mtoto katika makao ya mtoto anapewa chakula bora chenyelishe muafaka na yakutosha kwa kuzingatia umri wa mtoto na kwa kuzingatia viwango viliwyowekwa na Kamishna.

(2) Milo inayotolewa kwa watoto itakuwa milo kamili kwa ubora na itaandaliwa na kupikwa kwa usafi na kwa kuzingatia mazingira safi na vigezo vyta usafi.

(3) Chakula kitahifadhiwa vizuri ili kuzuia magonjwa.

(4) Watoto wenyewe mahitaji ya milo maalumu kutoekana na sababu za afya watakuwa na haki ya kupewa milo hiyo.

(5) Kila Mwenye Leseni ataandaa mchanganuo wa chakula bora kinachotolewa kwa watoto katika makao ya watoto na mchanganuo huo utakuwa tayari kwa ukaguzi wa afisa ustawi wa jamii na Kamati ya Ustawi wa Jamii.

(6) Maji safi ya kunywa yatatakiwa kuwepo kila wakati kwa ajili ya watoto.

Huduma za matibabu

**18.-**(1) Mwenye Leseni atahakikisha kwamba kila mtoto anachunguzwa na afisa afya kabla ya kumpokea mtoto katika makao na afisa wa afya atarekodi matokeo katika Fomu namba 8.

(2) Kama mtoto atakubaliwa kwa dharula, hitaji la kufanya uchunguzi wa kiafya katika kanuni ndogo ya (1) litatolewa na uchunguzi wa afya utafanywa mara moja baada ya

kupokelewa.

(3) Mwenye Leseni atahakisha kuwa kila mtoto anafanyiwa uchunguzi wa kiafya kwa kipindi kisichozidi miezi sita na, pale ambapo mtoto anayechunguzwa anasumbuliwa na maradhi ya kimwili au kiakili, afisa wa afya atawasilisha taarifa kwa Afisa wa Ustawi wa Jamii kuelezea chanzo na kiwango cha maradhi.

(4) Mwenye leseni atahakikisha kwamba watoto wanaoishi katika makao ya watoto-

- (a) wanapewa kinga dhidi ya ugonjwa huo kama afisa wa afya au Kamishna anaweza kuelekeza;
- (b) wanapata matibabu kama itakavyoelezewa na afisa wa afya;
- (c) wanapelekwa kliniki kila mwezi kama mtoto yuko chini ya umri wa miaka mitano; na
- (d) wanafanyiwa uchunguzi wa mara kwa mara wa meno na wanapata matibabu ya meno pale inapohitajika.

(5) Endapo mtoto ana umri mkubwa na ni mtu mzima, aina yoyote ya matibabu na uchunguzi ataelezwa mtoto baada ya kupata idhini yake.

(6) Meneja anaweza kutoa kibali cha kupewa matibabu kwa mujibu wa kifungu cha 138(1) cha Sheria, iwapo mtoto hataweza kutoa idhini au iwapo Meneja ataona kuwa matibabu ni kwa maslahi ya mtoto.

(7) Mtoto hatafanyiwa utafiti wa kitibabu bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa Kamishna-

- (a) mahali pa kutosha na pasafi pakulala ambapo patakuwa kwenye viwango vifuatavyo-
  - (i) kutakuwa na kitanda kinachofaa kwa mtoto;
  - (ii) kutakuwa na hewa ya kutosha na nafasi yenye umbali usiopungua futi mbili na nusu kati ya kitanda na kitanda, kitanda cha mtoto au kitanda cha mtoto mchanga vinavyotumiwa na watoto chini ya umri wa miaka sita;
  - (iii) kutakuwa na nafasi kwenye chumba isiyopungua futi arobaini kwa kila mtoto wa miaka sita au zaidi;
  - (iv) mtoto wa kiume aliyetimiza umri wa miaka minne hataruhusiwa kulala katika chumba

kimoja au bweni ambalo watoto wa kike ambaao wametimiza umri umri wa miaka mine au zaidi wanalala.

- (b) chumba cha matibabu kilichotengwa kitatolewa pale ambapo mtoto atakapo kuwa anasumbuliwa na magonjwa kuambukizwa atawekwa contagious, isipokuwa kwamba kwa madhumuni ya kifungu hiki ugonjwa wa kuambukiza hautajumuisha Virusi Vitokanavyo na Ukimwi;
- (c) kabati la peke yake, safi na vifaa rafiki kwa ajili ya mtoto wa kike na kiume vinavyotosheleza idadi ya watoto wanaoishi katika makao na angalau choo kimoja kwa kila watoto kumi na tano na choo cha kukaa kisichopungua mita 6 au futi 20 kwenda chini na utakuwa na mita 15(futi 50) kutoka katika shimo lililochimbwa;
- (d) sehemu safi na yenye hewa nzuri ya chumba cha kulia chakula ikiwa na meza za kutosha na viti vinavyofaa kwa watoto wanaoishi katika nyumba;
- (e) sehemu ya kufulia zilizotofautishwa kwa watoto wa kiume na watoto wa kike inayotosheleza idadi ya watoto wanaoishi katika makao;
- (f) choo kinachofaa kikiwa na vifaa muhimu vyaa kupikia;
- (g) sehemu ya kufulia ikiwa na vifaa vyaa kutosha;
- (h) vyandarua vilivyowekwa dawa kuzuia watoto dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kila mtoto;
- (i) vifaa vyaa burudani kama eneo la kuchezea,vifaa vyaa kutosha vyaa kuchezea kwa ajili ya kufundishia na vyaa kumkuzia mtoto, vifaa vyaa ndani na nje vyaa michezo ya watoto inavyofaa kwa umri wote;
- (j) eneo salama;na
- (k) choo kilichotenganishwa na vifaa vyaa kuoshea kwa wafanyakazi na wageni.
- (2) Mwenye leseni atahakikisha kwamba-
- (a) iwapo mkondo wa maji upo katika eneo lake,kama vile sehemu ya kuogelea na mashimo,zimewekwa uzio kwa usalama wa watoto;
- (b) sakafu ya eneo la kuchezea la nje halina vitu vyenye ncha kali,vitu vyenye sumu, mimea yenye madhara

- na vitu visivyo hitajika na vifaa;
- (c) kwamba vifaa vyote hatari na vyenye sumu vinawekwa mahala salama na ambapo havitafikiwa na watoto;
  - (d) matakataka yanatupwa salama na kwa utaratibu wa kiafya;
  - (e) watoto wanaoga na kupewa vifaa vingine vyakuoshea kila siku;
  - (f) vifaa vyakiafya vina kidhi viwango vyakafya na usafi na vinawekwa katika mazingira salama muda wote na vyoo vinapatikana usiku,lakini vikiwa vimetenganishwa
  - (g) na sehemu ya kulala;
  - (h) nguo zinazofaa, za kutosha na safi na zinazoendana na hali ya hewa zinatoleawa kwa watoto;
  - (i) kila mtoto anapewa mashuka safi ambayo yanabadilishwa kila baada ya wiki mbili na kubadilishwa mara kwa mara;na
  - (j) unakuwepo uangalizi maalumu wa mahitaji ya watoto wa kike na watoto wenyewe ulemavu na masharti mengine ya kimatibabu.

(3) Mwenye Leseni ya makao ya watoto ambayo inalaza watoto wenyewe ulemavu atahakikisha vifaa vinafikika na vinafaa kwa watoto wenyewe ulemavu na wenyewe mahitaji maalum na kwa pekee, watoto wenyewe ulemavu na mahitaji maalum wanaweza kufikia sehemu ya kuoshea, sehemu za kulala, chumba cha kulia chakula, vifaa vyakafya na maeneo ya burudani na vyoo vinavyofaa, na choo kimoja kinachofaa kwa watoto watano wenyewe ulemavu.

(4) Iwapo makao ya watoto yapo katika eneo ambalo lina gorofa moja, sehemu ya kulala na sehemu ya kulia chakula kwa watoto itatakiwa iwekwe chini, au kwa kibali cha Kamishna, iwe chini karibu na sehemu ya chini.

(5) Kila sehemu ya makao ya watoto itatakiwa kuwa safi na mazingira salama muda wote.

(6) Kila makao ya watoto itaweka vifaa vinavyofanya kazi vyakupambana na moto

(7) Kila makao ya watoto itakuwa na kisanduku cha huduma ya kwanza, ambacho kitakuwa na madawa ambayo ni salama kwa watoto.

Malazi na vifaa  
vingine

- 19.** Kila makao ya watoto yatakuwa na-
- (a) malazi safi na ya kutosha ambayo yatakuwa na viwango vifuatavyo-
- (i) uwepo wa kitanda kimoja kinachofaa kwa kila mtoto;
  - (ii) uwepo wa mwanga na hewa ya kutosha na eneo la lenye urefu usiopungua futi mbili na nusu kati ya vitanda, vitanda vyta watoto au vitanda vyta watoto wachanga vinavyotumiwa na watoto chini ya umri wa miaka sita;
  - (iii) kutakuwa na eneo la ndani ya chumba ambalo si chini ya futi arobaini za mraba kwa kila mtoto wa miaka sita au zaidi;
  - (iv) watoto wa kieme ambaao wametimiza umri wa miaka minne hawataruhusiwa kulala chumba kimoja au bweni moja na watoto wa kike waliotimiza umri wa miaka mine na zaidi;
- (b) chumba cha matibabu kilichotengwa kitawekwa kwa watoto wanaosumbuliwa na ugonjwa wowote wa kuambukiza au magonjwa ya kuambukiza kwa njia ya hewa na isipokuwa kama magojwa ya maambukizi hayatajumuisha Virusi vyta Ugonjwa wa UKIMWI;
- (c) sanduku la peke yake, safi na vifaa rafiki vyta kuchezza vyta mtoto kwa ajili ya watoto wa kieme na wakike vinayotosheleza na idadi ya watoto wanaoishi katika makao na angalau choo kimoja kwa watoto kumi na tano na choo cha shimo kisichopungua urefu wa mita 6 au wafuti 20 kwenda chini na kuwe na mita 15 (Futi 50) kutoka umbali wa kisima;
- (d) safi, yenye nafasi na hewa kwenye chumba cha kulia chakula ikiwa na meza na viti vinavyofaa kwa watoto wanaoishi katika makao;
- (e) kutofautisha vifaa vyta kufulia kwa ajili ya watoto wa kieme na wakike vinayotosheleza idadi ya watoto wanaoishi katika makao;

- (f) jiko linalofaa liwe na vifaa muhimu vya kupikia;
  - (g) sehemu ya kufulia yenye vifaa vya kufulia vya kutosha;
  - (h) vyandarua vilivyowekewa dawa kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya malaria kwa kila mtoto;
  - (i) vifaa vya burudani kama vile vifaa vya kuchezea kwa ajili ya kufundisha na malezi kwa ukuwaji wa watoto, vifaa vya ndani na nje kwa ajili ya michezo inayofaa kwa umri wote;
  - (j) maeneo salama; na
  - (k) choo na vifaa vya kutosheleza kwa ajili ya wafanyakazi na wageni.
- (2) Mwenye Leseni atahakikisha-
- (a) kwamba iwapo kutakuwa na maji katika eneo, kama vile bwawa la kuogelea na visima vya maji yanawekewa uzio kwa ajili ya usalama wa watoto;
  - (b) kwamba eneo la nje la kuchezea litakuwa halina vitu vyenye ncha kali, vitu vyenye sumu, mimea yenye madhara na vitu na vifaa visiviyotumika;
  - (c) kwamba vifaa vyote vya hatari na vitu vyenye sumu vinawekwa salama na kutofikiwa na watoto;
  - (d) kwamba takataka za nyumbani zinatupwa kwa utaratibu salama na kuzingatia usafi;
  - (e) kwamba kila siku watoto wanapewa vifaa vya kuogea na kufulia;
  - (f) vifaa vya usafi vina kidhi vigezo vya afya na usafi na vinawekwa katika mazingira ya usafi muda wote na kwamba choo kinafikika wakati wa usiku, lakini ikiwa imetofautishwa na sehemu za kulalia;
  - (g) watoto wanapatiwa nguo zinazofaa, zinazotosheleza na safi kulingana na hali ya hewa kwa watoto wote;
  - (h) kila mtoto atapewa mashuka ambayo yatakuwa yanabadilishwa si chini ya mara moja kila baada ya wiki mbili na mara kwa mara yanabadilishwa; na
  - (i) kipauambele maalumu kwa mahitaji yake binafsi yatolewe kwa watoto wa kike na kwa watoto wenye ulemavu au mahitaji mengine ya kitabibu.
- (3) Mwenye Leseni ya makao ya watoto ambazo zinalaza watoto wenye ulemavu atahakikisha kwamba vifaa vinapatikana na kupewa kwa watoto wenye ulemavu na mahitaji

maalum na hasa watoto wenyewe ulemavu na mahitaji maalum wanaweza kupata vifaa vya kufulia, maeneo ya kulala, chumba cha kulia chakula, vifaa vya afya na maeneo ya burudani na vyoo vinavyofaa na angalau choo kimoja kinachofaa kwa watoto watano na kwa watu wenyewe ulemavu.

(4) Pale ambapo makao ya watoto yapo katika majengo ambayo yana ghorofa zaidi ya moja, sehemu ya kulala na chumba cha kulia chakula kwa ajili ya watoto kitakuwa sehemu ya chini au, kwa idhini ya Kamishna, itakuwa sehemu inayofuata baada ya sehemu ya chini.

(5) Sehemu zote za makao ya watoto muda wote zitawekwa katika mazingira safi.

(6) Kila makao ya watoto yataweka mahali inapofaa vifaa vya kuzuua moto.

(7) Kila Makao ya Watoto yatakuwa na kifaa cha huduma ya kwanza, ambacho kitakuwa na madawa ambayo ni salama kwa watoto.

Elimu na  
mafunzo ya  
vitendo

**20.** Kila mwenye leseni ya makao ya watoto atahakikisha kwamba kila mtoto anapata elimu ya msingi na, kwa kadri inavyowezekana anapata elimu ya juu na mafunzo ya ufundi.

#### **SEHEMU YA SITA UUNGANISHAJI NA UONDOAJI**

Ziara na  
mawasiliano

**21.-(1)** Kwa nia ya kuwezesha kuunganishwa tena kwa mtoto na wazazi wake, walezi au ndugu kwa mujibu wa kifungu cha 137(3) cha Sheria, mfanyakazi wa Makao ya Watoto atachukua hatua zinazofaa kuwezesha utembeleaji wa wazazi, walezi, ndugu na marafiki wa mtoto na atashirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii kwa madhumuni haya.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), makao ya watoto yanaweza kuamua kuweka muda maalum na siku za kutembelewa na wageni kwa ajili ya kuweka usimamizi mzuri wa taasisi lakini kutembelewa huko na wageni hakutaruhusiwa kwa zaidi ya mara tatu kwa wiki na si chini ya masaa mawili kwa kila muda wa kutembelewa.

(3) Watoto nao wataruhusiwa kuwatembelea wazazi, walezi, ndugu na marafiki isipokuwa kama afisa ustawi wa jamii wa makao wanayoishi wametathmini madhara yanayoweza

kutokea kabla ya mtoto hajatembelea nyumba na kuamua kwamba kutembelewa huko ni kwa maslahi ya mtoto.

(4) Mtoto ambaye umri wake ni chini ya miaka kumi na mbili atatakiwa kuambatana na mmoja kati ya mfanyakazi wa malezi ya makao anapotembelea mtu nje ya makao ya kulelea.

(5) Kwa mujibu wa kifungu cha 137(3) cha Sheria, Afisa Ustawi wa Jamii anatembelea mara kwa mara kwenye nyumba za wazazi, ndugu au walezi na kutoa msaada unaofaa kwa ajili ya kuwaunganisha.

Maandalizi ya  
kuwaunganisha  
na kuwatoa  
watoto

**22.-**(1) Afisa Ustawi wa Jamii atapitia kwa kipindi mpangilio wa mtoto katika makao ya watoto kuhakikisha kwamba mpangilio huo ni kwa maslahi ya mtoto.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 137(3) cha Sheria, mtoto atapewa msaada wa kisaikolojia kwa ajili ya kumuandaa, kimwili, kifikra, kijamii, kitamaduni na kiakili kumsaidia kumrudisha kwenye familia na kumunganisha na jamii.

(3) Kadri itakavyowezekana na kwa maslahi mazuri ya mtoto, mtoto ataunganishwa na watoto au walezi na kwa masharti kuwa:

- (a) meneja wa Makao ya Watoto, afisa ustawi jamii na mwangalizi wa mtoto atamsaidia afisa ustawi wa jamii kufanya kazi na wazazi, walezi na ndugu, kuandaa na kutekeleza mpango wa kumrudisha ili kusaidia mtoto kuanganishwa na wazazi, walezi au ndugu, pale inakavyowezekana;
- (b) mpango wa kumrudisha mtoto utaweka utaratibu kwa mtoto wa kutembelewa katika nyumba ya mtoto kabla ya kuanganishwa;
- (c) katika kufanya maandalizi na utekelezaji wa mpango wa kuwaunganisha, maoni ya mtoto yatahakikishwa, kama mtoto anaweza kuelezea maoni yake na maoni yake yatachukuliwa kwa uzito kwa kuzingatia umri wa mtoto uelewa;
- (d) hakuna mtoto atakaye unganishwa na wazazi, walezi mpaka taarifa ya uchunguzi ifanywe na Afisa Ustawi wa Jamii na kuhakikisha kuwa kumrudisha ni kwa maslahi ya mtoto;
- (e) katika kufanya tathmini inayotakiwa na kanuni

ndogo ya (3)(d), wazazi na walezi watakaongoza kuunganishwa tena na mtoto na utayali wa kumpokea na kutunza mtoto.

(4) Pale ambapo kumrudisha tena kwa mtoto hakuwezekani, Meneja na Afisa Ustawi wa Jamii wa sehemu anayoishi atashirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii, kutafuta njia mbadala ya kumlea mtoto nje ya taasisi.

(5) Pale ambapo mtoto anaweza kutoa maoni yake, mtoto atashauriwa juu ya njia mbadala ya kuendelea kumtunza na maoni yake yatapewa uzito kwa kuzingatia umri wa uelewa wa mtoto.

(6) Pale ambapo inafaa na inapowezeekana, Afisa Ustawi wa Jamii ataomba kibali cha wazazi na walezi kwa ajili ya njia kumhamisha mtoto sehemu ya kutunza, na anapotaka kubadilisha mlezi wa kambo, kibali kitatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Malezi ya Kambo za mwaka 2011.

(7) Endapo mtoto atatimiza miaka 18, Makao ya Watoto yatamuanda mtoto kujitegemea na Afisa Ustawi wa Jamii atashirikiana na makao ya watoto kupata malazi na ajira au kujiendeleza kielimu au mafunzo ya ufundi kwa kushirikiana na mtoto.

(8) Bila ya kujali kanuni ndogo ya (7) kama mtoto ana ulemavu ikimaanisha kwamba mtoto hataweza kuishi peke yake, Afisa Ustawi wa Jamii atashirikiana na makao ya watoto kuonyesha mpango wa matunzo.

(9) Pale ambapo mtoto anatoroka kwenye makao ya watoto, Meneja wa makao hayo ya watoto atamueleza Afisa Ustawi wa Jamii ndani ya masaa 48.

Kutolewa

**23.-(1)** Mtoto hataondolewa kwenye makao ya watoto bila ya kibali cha Afisa Ustawi wa Jamii, isipokuwa kama mtoto ametimiza umri wa miaka 18.

(2) Kibali kitatolewa bila ya kuchelewa, katika fomu iakayayotambulika kama Form No.9, isipokuwa kama Afisa Ustawi wa Jamii ataamua kwamba kutolewa huko sio kwa maslahi ya mtoto.

(3) Meneja atahakikisha kwamba tarehe na sababu ya kuondolewa zinarekodi katika Daftari la kupokea na kuondoa mtoto.

**SEHEMU YA SABA  
USIMAMIZI WA TABIA ZA MTOTO**

Usimazi wa  
tabia

**24.**-(1) Kila Meneja wa makao ya watoto ataendeleza juhudzi za kutengeneza mazingira ambayo yatatumbua muda wa mtoto kwa utaratibu unaofaa na unaojenga, ambao utaendeleza tabia chanya na yenye manufaa na ambayo itaenda sambamba na mila na desturi za jamii.

(2) Meneja na wafanyakazi wa makao ya watoto wataendeleza nidhamu nzuri kwa-

- (a) kuhakikisha kwamba watoto wanapatiwa ujuzi na msaada ambao utasaidia kuwa na tabia zinazojenga na zinazofaa kwa jamii;
- (b) kuonyesha tabia zinazotakiwa kwa kuwa mfano katika tabia na mahusiano na watoto;
- (c) kuhakikisha, kwa kuitia programu na mfano unaofaa, kwamba watoto wamepewa fursa na kutiwamoyo kwa kuonyesha kwa vitendo tabia njema; na
- (d) kuweka mfumo wa haki na endelevu ambao utaleta tabia zinazofaa na kuonyesha madhara ya tabia mbaya.

Hatua za  
kinidhamu

**25.**-(1) Mtoto ambaye anakiuka Kanuni zozote za tabia kwenye Makao ya Watoto kama ilivyotolewa chini ya Jedwali la Tatu atachukuliwa hatua za kinidhamu.

(2) Kama mfanyakazi wa makao anasababu za msingi kwamba mtoto anatenda au ameonyesha vitendo vya utovu wa nidhamu, mara moja atamtaarifu Meneja au Afisa Mfawidhi kwa mdomo au kwa maandishi juu ya-

- (a) vitendo vya utovu wa nidhamu ambavyo anashutumiwa kuwa amezitenda; na
- (b) mazingira yanayopelekea vitendo vya utovu wa nidhamu.

(3) Kabla ya kuamua kama hatua za kinidhamu zimechukuliwa meneja-

- (a) ataelezia kwa mtoto shutuma katika lugha inayofaa kulingana na umri wa mtoto na kiwango cha uelewa;
- (b) atamruhusu mtoto kuwasilisha utetezi na kuelezea maoni yake kuhusu kitendo kibaya alichokitenda.

(4) Pale Meneja au Afisa Mfawidhi ameridhishwa kwamba mtoto amekiuka miiko ya makao ya watoto, Meneja au Afisa Mfawidhi anaweza kuamrisha moja au zaidi ya hatua za kinidhamu zifuatazo-

- (a) kutochukua hatua;
- (b) onyo au kalipio;
- (c) msamaha wa mdomo au maandishi;
- (d) kusitisha kwa muda au moja kwa moja au kutoa vipaumbele zaidi au shughuli za kawaida zinazotolewa kwa mtoto;
- (e) kazi za ziada au shughuli nyingine,kwa kipindi maalum kisichozidi masaa mawili;
- (f) kumuhamisha mtoto kwenye chumba tofauti au sehemu ya chumba cha kuishi kwenye Makao ya Watoto.

(5) Mtoto anahaki ya kuhoji utolewaji wa adhabu au hatua za kinidhamu kwa kuwasilisha malalamiko yake kwa mujibu wa Kanuni ya 30 ya Kanuni hizi.

(6) Kitendo chochote cha tabia mbaya kinachopelekea kuchukuliwa kwa hatua za kinidhamu kama ilivyowekwa katika kanuni ndogo ya (4)(d),(e) na (f) kitaandikwa katika Kitabu cha Usimamizi wa Tabia na kitakachowekwa katika Makao ya Watoto.

(7) Hatua zifuatazo za kinidhamu zimezuiliwa-

- (a) adhabu ya mwili;
- (b) adhabu ya kikudi kwa tabia ya mtu mmoja;
- (c) udhalilishaji, unyanyasaji wa kiakili au udhalilishaji wa kutumia maneno;
- (d) kunyimwa au kumpunguzia haki za msingi kama vile chakula, nguo au uangalizi wa matibabu;
- (e) kukataliwa au kuzuiwa kutembelewa,kupiga simu au kuwasiliana na familia na watu wengine muhimu;
- (f) kuondolewa shulenii au kwenye programu za mafunzo ya ufundi;
- (g) kufungiwa peke yake;
- (h) kushikiliwa.

Uzuiaji wa  
matumizi ya  
nguvu

**26.-**(1) Nguvu haitatumika kama sehemu ya adhabu dhidi ya mtoto.

(2) Matumizi ya nguvu yanaweza kutumika tu katika

mazingira maalum iwapo itatakiwa-

- (a) umzuia mtoto kuumia mwenyewe au wengine au kusababisha maramoja au uharibifu mkubwa wa mali;na
- (b) namna nyingine ya kumshughulikia na mtoto bila ya kutumia nguvu kumeshindikana au hazilingani na mazingira.
- (3) Pale ambapo nguvu inatumika dhidi ya mtoto, kiwango cha nguvu kitalingana na hakitazidi kwa kuzingatia aina ya karipio lililowekwa kwa mtoto na mazingira yoyote ya kesi.
- (4) Matumizi ya nguvu yatatumika kwa afisa aliyefunzwa.
- (5) Kushikiliwa kwa mtoto kutakako sababisha kushindwa kupumua kunazuiliwa na vitendo vingine vyoyote ambavyo lengo lake ni kusababishia maumivu kwa mtoto.
- (6) Matumizi yoyote ya nguvu au zuio dhidi ya mtoto na afisa yataarifiwa maramoja kwa msimamizi wa makao na kuingizwa katika rejista ya kuthibiti tabia ya watoto.

**SEHEMU YA NANE**  
**UFUATILIAJI, UKAGUZI NA MALALAMIKO**

Ufutiliaji na  
ukaguzi

**27.-**(1) Kamishna ataweka kumbukumbu zote za makao ya watoto na taarifa za mtoto anayeishi, aliyeingizwa na kuondolewa kutoka katika Makao ya Watoto kulingana na umri wao, jinsi na sababu za kuondolewa na pia watoto wenye ulemavu watakavyowekwa katika Makao ya Watoto.

(2) Kwa mujibu wa kifungu cha 136 na kifungu cha 151(1) cha Sheria, Makao yote ya Watoto yatakaguliwa ili kuhakikisha kuwa viwango vya huduma, malezi na ulinzi wa mtoto, majengo, huduma na vifaa, vitabu, mahesabu na kumbukumbu nyingine zinakidhi mahitaji yaliyowekwa na Kanuni hizi.

(3) Kamishna atahakikisha kwamba ukaguzi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) unafanywa angalau maramoja kila baada ya miezi sita.

(4) Ukaguzi unaofanywa chini ya kanuni ndogo ya (2) utafanywa na Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ambapo makao ya watoto yapo, isipokuwa kama Kamishna atamteua Afisa

Ustawi wa Jamii kutoka katika kitengo kufanya ukaguzi au kumteua mtu mwingine, chombo au taasisi kufanya ukaguzi, na katika jambo hilo, hakuna ukaguzi utafanyika na mtu yeyote au taasisi ambayo ina mgongano wa maslahi, ikijumuisha maslahi ya kifedha katika makao ya watoto, au na mtu yeyote ambaye mjambe wa kamati ya ustawi, au ambaye ana familia ambayo ina maslahi katika makao ya watoto au Kamati ya Ustawi.

(5) Kila ukaguzi utakaofanyika utaambatana na taarifa ya maandishi, inayojumuisha mapendekezo yoyote yaliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (6) na itapelekwa kwa Kamishna na Mwenye leseni ya Makao ya Watoto, na katika jambo ambalo ukaguzi umefanywa na mtu ambaye si Afisa Ustawi wa Jamii, kwa Afisa Ustawi wa Jamii katika Wilaya ambayo Makao ya Watoto yapo.

(6) Katika jambo ambalo makao ya watoto yako chini ya kiwango kinachohitajika na kanuni hizi, taarifa itakuwa na maelekezo ya hatua kwamba Mwenye leseni na Meneja atatakiwa kuchukua kukidhi viwango.

(7) Makao ya watoto yatapewa si chini ya miezi miwili na si zaidi ya miezi sita kutekeleza maagizo ya kutekeleza maelekezo, kulingana na ukubwa wa maagizo na hasa hasa haja ya kutoa kipindi maalum cha kufanya marekebisho ya majengo ya eneo.

(8) Wakati wa kufanya ukaguzi, Afisa Ustawi wa Jamii au mtu au chombo kilichoteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (4) atatathimini iwapo maelekezo yametekelizwa.

Ukaguzi makao  
ya watoto baada  
ya kupata  
malalamiko

**28.-(1)** Katika nyongeza ya mamlaka aliyonayo Kamishna chini ya kifungu cha 136 na kifungu cha 151(1) cha Sheria, Kamishna anaweza kufanya au kuelezea kufanyika kwa ukaguzi mara baada ya kupokea malalamiko yoyote kuhusiana na Makao ya Watoto au baada ya kupata taarifa yoyote ambayo inaonyesha ukiukwaji wa Kanuni hizi na atatoa maelekezo ya namna gani Mwenye leseni au Meneja atatatu taarifa ya ukaguzi huu.

(2) Makao ya watoto yatapewa fursa ya kutekeleza maelekezo yaliyotolewa chini ya kanuni hii na Kanuni ya 27(5) ya Kanuni hizi, isipokuwa pale ambapo mwenye leseni anashindwa kufuata maelekezo kwa muda au Pale Kamishna anapoamini Mwenye Leseni hatafuata maelekezo au anakiuka

Kanuni unatosha kusababisha madhara makubwa kwa mtoto au mtoto anakuwa katika hatari ya kupata madhara, Kamishna atafuta leseni kwa mujibu wa kifungu cha 140 cha Sheria.

Miongozo ya  
Malalamikoo

**29.-**(1) Kamishna atatoa miongozo ya jinsi ya kushughulikia malalamiko na maombi kwa ajili ya kupitia tena malalamiko ya maombi.

(2) Mwenye leseni atahakikisha kuwa nakala za miongozo ya malalamiko zinatolewa kwa watoto wote baada ya kukubaliwa kuishi kwenye makao ya kulelea watoto na nakala itapatikana pale itakapoomba na mzazi au mlezi wa mtoto.

Haki ya  
kulalamika

**30.-**(1) Mtoto anayetunzwa katika Makao ya Watoto anaweza kulalamika kuhusu jambo lolote linalohusu malezi au anavyohudumiwa.

(2) Malalamiko kuhusu kuhudumiwa kwa mtoto husika linaweza kufanywa na mwakilishi wa mtoto au mtu ye yeyote mwenye maslahi.

(3) Malalamiko yanaweza kufanywa kwa mdomo au kwa maandishi kwa mmoja au zaidi ya watu wafuatao-

- (a) Meneja wa makao;
- (b) Kamati ya ustawi;
- (c) Afisa Ustawi wa Jamii;
- (d) Kamishna;
- (e) Afisa mtendaji wa mtaa/kijiji;
- (f) Afisa mtendaji wa kata;

(4) Mtoto anaweza kutoa malalamiko kwa mdomo au maandishi.

Kumbukumbu  
ya malalamiko

**31.** Malalamiko yote yatachunguzwa na kutatuliwa au kushughulikiwa kwa muda na mtoto atatarifiwa matokeo kwa mujibu wa utaratibu wa Mwongozo wa Malalamiko.

Daftari la  
malalamikoo

**32.-**(1) Meneja atatunza rejestaa la malalamiko yenyeye taarifa za malalamiko yote yaliyofanywa na au kwa niaba ya mtoto, isipokuwa kwa malalamiko ambayo mtoto hatataka yaandikwe kwenye rejestaa.

(2) Taarifa zifuatazo zitaandikwa kwenye kila lalamiko-

- (a) tarehe ambayo malalamiko limefanywa;
- (b) jina la mlalamikaj;

- (c) mambo ya msingi kwenye lalamiko;
- (d) maelezo mafupi kuhusu taratibu za kufuatwa wakati wa kushughulikia malalamiko; na
- (e) uamuzi au suluhisho lililotolewa kuhusiana na lalamiko.

(3) Rejesta ya malalamiko itapatikana kwa ajili ya kukaguliwa na Kamishna, Afisa ustawi wa jamii, Kamati ya ustawi au mamlaka yoyote inayotekeleza majukumu yake.

**SEHEMU YA TISA  
MASHARTI YA JUMLA**

Taarifa ya kifo

**33.**-(1) Kila Mwenye leseni atamtaarifu Afisa Ustawi wa Jamii juu ya kifo cha mtoto yeoyote ambaye anaishi kwenye Makao ya watoto ndani ya masaa ishirini na nne toka kutokea kwa kifo hicho na taarifa hiyo itataja jina, jinsia na umri wa mtoto aliyefariki na tarehe, sababu na mazingira ya kifo.

(2) Mwenye leseni, baada ya kutokea kifo cha mtoto na kwa kushauriana na Afisa Ustawi wa Jamii, atapewa cheti cha kifo na ripoti ya daktari ya taarifa ya uchunguzi ya chanzo cha kifo kama itatakiwa.

(3) Iwapo mzazi au mlezi anamfahamu Afisa Ustawi wa Jamii atamtaarifu ndani ya masaa 24 baada ya kutokea kifo cha mtoto.

(4) Kamati ya Ustawi wa Jamii itapokea taarifa ya kifo cha mtoto na itazingaia sababu ya kifo cha mtoto na kama kuna hatua zozote zinatakiwa kuchukuliwa na makao ya watoto katika kurekebisha utaratibu wake na utendaji.

Taratibu  
mbadala kwa  
mtoto baada ya  
kufutwa kwa  
leseni

**34.** Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 140(2) cha Sheria-

- (a) Kamishna na Afisa Ustawi wa Jamii anaweza kuweka taratibu mbadala wa malezi ya watoto wanaoishi katika makao ya watoto;
- (b) wakati wakumbadilisha mtoto kwenye malezi mbadala atazingatia haki za mtoto ya kuwasiliana na familia yake;
- (c) mtoto atashilikishwa wakati wa kumbadilisha sehemu nyingine kama mtoto anaweza kutoa maoni yake,kabla ya uamuzi kufanywa,na maoni yake

yatachukuliwa kwa kuzingatia umri wa mtoto na uelewa wake.

Masharti ya  
mpito

**35.** Kila makao ya watoto iliyopo yatatakiwa kufuata masharti ya Kanuni hizi mara baada ya kutangazwa isipokuwa kwa Kanuni za 8, 10 na 19 ambazo atatakiwa kuzifuata ndani ya miezi ishirini na nne baada ya kuanza kwa kutumika kwa Kanuni hizi.

Mamlaka  
kutengeneza  
fomu na  
taratibu

**36.** Kamishna ataandaa fomu na taratibu za utekelezaji wa Kanuni hizi.

**JEDWALI LA KWANZA**

---

**WAFANYAKAZI WA MALEZI/UWIANO WA MTOTO**

---

*(Imeandalisha chini ya kanuni ya 10(3))*

---

| MUDA WA MCHANA |                      |                 | MUDA WA SIKU                   |                 |
|----------------|----------------------|-----------------|--------------------------------|-----------------|
| Umri wa mtoto  | Idadi ya wafanyakazi | Idadi ya watoto | Idadi ya wafanyakazi wa malezi | Idadi ya watoto |
| 0-6            | 1                    | 5               | 1                              | 5               |
| 7-14           | 1                    | 10              | 1                              | 20              |
| 15-17          | 1                    | 10              | 1                              | 25              |

**JEDWALI LA PILI**

---

**MAADILI**

---

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

---

Mimi, Jina ..... Cheo ..... nakubali kuzingatia kwa hali ya juu viwango binafsi na vya kitaaluma katika utendaji wangu kila mara, katika mahusiano yangu na watoto katika makao ya watoto:

- (a) nitalinda na kutunza watoto dhidi ya vitendo vyovoyote vya ukatili, unyanyasaji, unyonyaji, maonevu na kutelekezwa;
- (b) nitawahudumia watoto kwa heshima bila kujali rangi, jinsia, lughu, dini, mtazamo wa kisiasa, utaifa, kabilia, mali, ulemavu, hali ya afya, kuzaliwa au hali nyingine yejote;
- (c) sitabagua, sitaonyesha tofauti katika huduma au sitompendelea mtoto mmoja na kuwabagua wengine;
- (d) sitatumia lughu au kuonyesha tabia isiyo njema kwa watoto, sitawagombeza sitawatukana, sitawapahamasa ya ngono au vitendo kinyume na utamadun;

- (e) nitaheshimu hali ya utu wa watoto wote;
- (f) sitajihuisha kimapenzi na mtoto yelete, ikiwa ni pamoja na shughuli za ngono au ngono za kulipwa;
- (g) kamwe sitaonyesha tabia ambayo itaamsha hisia za ngono au kuonyesha tabia yelete mbaya kwa namna yelete ile;
- (h) kamwe sitafanya vitendo vyovoyete vile kwa nia ya kuwadharisisha, kuwatenga, kuwashushia hadhi ya watoto au kwa namna yelete ile kuchochera hisia ovu;
- (i) kamwe sitajihuisha kwa namna yelete ile katika unyonyaji wa watoto au kuwaweka watoto katika mazingira hatarishi kwa unyonyaji;
- (j) kamwe sitakuwa na mahusiano na watoto ambayo kwa namna yelete yanaweza kuchukuliwa kuwa ya kinyonyaji au ya kienevu au kufanya kitendo chochote kinachomuweka mtoto katika hatari ya kunyanyaswa;
- (k) kamwe sitakubaliana au kushiriki katika tabia ambazo ni kinyume na sheria na si salama au ni vyakinyanyasaji kwa mtoto;
- (l) nitajizuia kuangalia, kumiliki, kutengeneza picha za watoto za ngono;
- (m) nitaheshimu faragha ya watoto na kamwe sitapiga picha au video za watoto bila ridhaa yao au ridhaa ya meneja;
- (n) sitamkaribisha mtoto aliye peke yake nyumbani kwangu isipokuwa pale ambapo mtoto yupo katika hatari ya kuumizwa au kudhurika;
- (o) nitajizuia kukodi watoto kwa ajili ya kazi za ndani ambazo ni kinyume kwa kuzingatia umri au hatua za maendeleo ambazo zitaingilia muda wa watoto wa masomo na muda wa mazoezi au kuwaweka watoto katika hatari za kuumizwa;
- (p) nitazingatia sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni pamoja na sheria zinazohusu Sheria za Watoto; na
- (q) nitatoa taarifa kwa wakati kuhusu malalamiko au tuhuma za vitendo vya kikatili vya kinyanyasaji au vya kinyonyaji kwa mtoto kwa kuzingatia kanuni na utaratibu muafaka.

Ninaelewa kwamba wakati wa kutekeleza majukumu yangu ninawajibu wa kutumia busara na kuepuka vitendo na tabia ambazo zinaweza kutafsiriwa kuwa ni vya kinyanyasaji, vya kinyonyaji au hatarishi kwa mtoto.

Saini .....

Tarehe .....

**JEDWALI LA TATU**

---

**KANUNI ZA TABIA**

---

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 25(1)*

---

Watoto wote katika nyumba ya kulelea watoto wanatarajiwa kuwa na tabia njema na heshima kwa mujibu wa kanuni za maadili. Mtoto ye yote ambaye tabia yake itakiuka kanuni hizi anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

1. Kushirikiana na wafanyakazi lazima kufuata maelekezo yanayotolewa na wafanyakazi. Hii ina maana kwamba kuzungumza kwa kificho, kubeza, kudharau au kukiuka amri ya wafanyakazi hakuturuhusiwa.
2. Tumia lugha safi naya heshima kila wakati kwamba nyumba ya kulelea watoto hatavumilia lugha za kuapiza na matusi.
3. Kuonyesha uaminifu na uadilifu. Hata danganya au kutoa maelezo ya uongo kwa wafanyakazi.
4. Atawatendea wenzake kwa utu na heshima kama vile ambavyo angependa yeye kutendewa. Hii ina maana kwamba hakutakuwa na kubezana, kuitana majina, kutishana, kutaniana vibaya, kukalipiana au kutiana hasira au kupigana. Wakazi wote wanatakiwa kuzingatia haya ili waweze kuishi pamoja kwa amani.
5. Ataheshimu mali na vifaa vya wenzake. Hataharibu au kuiba mali ya mtu mwengine.
6. Mali na thamani za nyumba za watoto zitakuwa kwa ajili ya matumizi ya wote hivyo zinapaswa kulindwa. Hazitaharibwa au kutumiwa vibaya.
7. Ataruhusiwa kuwa na baadhi ya vitu vyake binafsi lakini havitatakiwa kuwa vya hatari kuwa usalama, ulinzi au amani ya nyumba ya kulelea watoto. Hataruhusiwa kumiliki kitu chochote isipokuwa akipata idhini ya meneja.
8. Kutengeneza au kumiliki silaha au kitu chochote ambacho kinaweza kusababisha madhara kutadhuiliwa.
9. Kama anahitaji matibabu kutokana na hali ya afya atapewa idhini na meneja kupata matibabu. Hataruhusiwa kuwa na dawa ambazo hadhija dhinishwa na meneja na hatampatia mtoto mwengine dawa.
10. Uvutaji sigara, utumiaji madawa na unywaji pombe unazuiliwa. Mtoto anaweza kupimwa wakati wowote ile kutambua kama ametumia madawa au kileo na hatakataa kupimwa.

11. Hataruhusiwa kupiga simu yejote isipokuwa kwa ruhusa ya meneja. Simu za mikononi na kadi za simu za mikononi hazitaruhusiwa.
12. Hataruhusiwa kufanya mapenzi na mtu yejote au kuonyesha tabia zozote zisizo za mapenzi. Hii inaweza kujumuisha kitu chochote kama kushikana, kusiko faa au busiana au kufanya ngono.
13. Kushirikiana na kuwasaidia wafanyakazi katika kulinda amani na nidhamu. Hatafanya kitu chochote kuvunja amani na nidhamu katika nyumba na kuhamasisha watoto wengine kufanya hivyo.
14. Hataruhusiwa kwenda nje ya mipaka ya nyumba au kwenye eneo lolote lililozuiliwa ndani ya nyumbani isipokuwa tu akipata idhini ya kufanya hivyo kutoka kwa meneja.

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

### **JEDWALI LA NNE**

---

FOMU

---

C.H. FOMU NA.1

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO, 2011

**REJISTA YA MAKAO YA WATOTO**

*Kanuni ya 6(1)*

---

| Na ya leseni | Jina la mwenye | Jina la makao | Wilaya | Kata | Uwezo wa juu ya makao |            |       | Jinsi ya watoto | Mahitaji | Tarehe ya leseni |
|--------------|----------------|---------------|--------|------|-----------------------|------------|-------|-----------------|----------|------------------|
|              |                |               |        |      | 0-6 miaka             | 6-17 miaka | Jumla |                 |          |                  |
|              |                |               |        |      |                       |            |       |                 |          |                  |
|              |                |               |        |      |                       |            |       |                 |          |                  |
|              |                |               |        |      |                       |            |       |                 |          |                  |
|              |                |               |        |      |                       |            |       |                 |          |                  |
|              |                |               |        |      |                       |            |       |                 |          |                  |
|              |                |               |        |      |                       |            |       |                 |          |                  |

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO

C.H. FOMU NA.2(a)

MAOMBI YA LESENI (*Mwombaji binafsi*)

(*Kanuni ya 5(2)*)

---

**1. Taarifa za Mwombaji**

- 1.1 Jina: .....
- 1.2 Anwani ya mahali: .....
- 1.3 Anwani ya posta: .....
- 1.4 Simu: .....
- 1.5 Simu ya mkononi: .....
- 1.6 Anwani ya barua pepe: .....
- 1.7 Je mwombaji anaendesa au awemewahi kuendesha nyumba ya kulelea watoto Tanzania  
NDIO ..... HAPANA .....
- Kama NDIO toa taarifa hapa chini  
Namba ya leseni ..... Namba ya Nyumba Wilaya inatumika?  
.....

NDIO/HAPANA

NDIO/HAPANA

- 1.8 Je mwombaji aliwahi kukataliwa leseni kuendesha nyumba ya kulelea watoto Tanzania;  
au je aliwahi kufutiwa leseni?

NDIO ..... HAPANA .....

Kama NDIO toa taarifa hapa chini

Namba ya nyumba Wilaya ..... Tarehe ya maombi/kufutwa  
.....

.....

**2. Taarifa za makao**

- 2.1 Jina la makao: .....
- 2.2 Wilaya: .....
- 2.3 Kata: .....
- 2.4 Anwani ya mahali: .....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

- 2.5 Anwani ya posta: .....

2.6 Simu: .....

2.7 Simu ya mkononi: .....

2.8 Anwani ya barua pepe: .....

2.9 Jina la meneja wa makao: .....

2.10 Ni kiasi gani cha uwezo wa juu unaokusudiwa wa makao (kwa mambo yote mawili).  
Umri miaka 0-6 ..... Umri miaka 7-17 .....

2.11 Watoto wa jinsi gani watacaa katika nyumba **MVULANA/MWANAMKE/WOTE**

2.12 Je nyumba ya kulelea watoto inakusudiwa kutunza watoto wenye ulemavu, magonjwa sugu au virusi vya ukimwi ambao watahitaji mahitaji maalum? **NDIO/HAPANA**  
Kama **NDIO** toa ufanuzi .....

2.13 Je majengo ya makao yanamilikiwa au yamekodiwa?  
Kama yamekodiwa, ni kwa muda gani na taarifa ya kusitisha ni muda gani?  
**YANAMILIKIWA/YAMEKODIWA**  
(kama yamekodiwa) muda wa pango ..... muda wa taarifa ya kusitisha pango .....

2.14 Vyanzo vya mapato kwa ajili ya makao:

### 3. Wadhamini

- ### 3.1 Toa taarifa za wadhamini watatu

Jina

Wadhifa

Mawasiliano

## 4. Tamko

- 4.1 Mimi, niliyeweka saini hapo chini nawasilisha fomu hii ya maombi ya leseni ya kuendesha nyumba ya kulelea watoto kwa msingi wa taarifa nilizotoa hapo juu. Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa niza kweli na saini na kama nikipewa leseni naahidi kuzingatia kanuni hizi na miongozi yoyote itakayotolewa na kamishna wa ustawi wa jamii.

Saini:.....

Jina la mwombaji : .....

Tarehe: .....

## Kanuni za Makao ya Watoto

---

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO, 2011

(TANGAZO NA ..... LA 2011)

CH FOMU NA.2(a)

TAARIFA YA UCHUNGUZI WA KIJAMII

(*Kanuni ya 16(5)*)

---

### 5. Taarifa ya Mtoto

- 5.1 Jina Kwanza:..... Jina la Pili:..... Jina la Mwisho:.....  
5.2 Tarehe ya kuzaliwa: ..... 1.3 Jinsia:.....  
1.4 Mkoa: ..... 1.5 Kabilia:.....  
1.6 Sehemu ya Makazi ya sasa/Taarifa ya Mawasiliano:  
.....

### 2. Vyanzo vya Taarifa

Taja vyanzo vya taarifa zinazotumika katika kufanya tathmini, na kama inafaa tarehe  
.....

- 2.1 Mazungumzo na mtoto: .....  
tarehe:.....  
2.2 Mazungumzo na mzazi wa mtoto/mlezi ..... tarehe: .....  
(Toa maelezo ni ya yupi).....

KIBALI CHA AFISA WA USTAWI WA JAMII KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA  
18 AU KIFUNGU CHA 137(1) KUHAMISHWA

JINA LA AFISA WA USTAWI WA JAMII

TAREHE:

Saini ya Afisa wa Ustawi wa Jamii

.....

### 3. Vyanzo vya taarifa

- 2.3 Maelezo/kukutana na Polisi:.....(tarehe)

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

- 2.4 Maelezo/kikao na Daktari:.....(tarehe)  
2.5 Maelezo/kikao na Nyumba ya Kulelea Watoto:.....(tarehe)  
2.6 Mengineyo (toa maelezo): .....

### **4. Familia ya sasa/hali ya uangalizi**

- 3.1 Hali ya sasa ya wazazi wa mtoto  
Baba:  
.....ANAISHI/AMEKUFA/HAJULIKANI(HAONEKANI)  
Mama:  
.....ANAISHI/AMEKUFA/HAJULIKANI(HAONEKANI)
- 3.2 Iwapo mzazi ana ndoa au hana ndoa?:.....  
3.3 Utaratibu upi wa sasa wa kumtunza mtoto? .....

### **5. Mahitaji ya mtoto**

- 4.1 Kama mtoto anahudhuria shule/mafunzo kwa sasa ..... Ndio/Hapana  
Kama ndio toa maelezo (Aina ya shule/kiwango).....  
4.2 Mtoto ana mahitaji yoyote ya elimu?  
.....  
4.3 Mtoto ana ulemavu, magonjwa sugu au mahitaji mengine yanayohitaji uangalizi  
maalumu ....Ndio/hapana    Kama Ndio, toa maelezo: .....

### **6. Kuunganishwa na familia**

- 5.1 Mtoto ametenganishwa na wazazi wake? Kama Ndio, kwa kipindi gani? .....
- 5.2 Jitihada gani zimetumika kutafuta wazazi/kumrudisha mtoto?  
.....  
.....  
5.3 Tathimini yako ni nini ya umuhimu wa familia kuunganika?  
.....  
.....

### **6. Tathimini ya Makao ya Watoto**

- 6.1 Tathmini yako ni kwanini inafaa kumpeleka mtoto kwenye nyumba ya kulelea watoto?  
.....  
6.2 Umeweza kuainisha umuhimu wa Makao ya watoto? ..... Ndio/Hapana

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

Kama ndio toa maelezo (kila nyumba ya kulelea watoto lazima iwe na leseni na kuingizwa katika Daftari – kwa kutumia Fomu ya Maombi (1a au b) na Tathimini na maamuzi Fomu (1c) kwa madhumuni haya)

Jina la Nyumba ..... Namba ya leseni .....

6.3 Kwanini unaamini kuwa nyumba ya kulelea watoto inayopendekezwa inafaa kwa mtoto

.....

6.4 Maoni yako kwa mtoto ni yapi?

.....  
.....

6.5 Nini maoni ya umuhimu wa Makao ya watoto?

.....  
.....

6.6 Kuna hitaji lolote la msaada kwa ajili ya kuhamishwa kwa mtoto? Kama Ndio/toa maelezo

.....

6.7 Hatua gani zaidi zinapaswa kuchukuliwa kama suluhisho la muda mrefu kwa mtoto huyu?

.....

### **7. Mapendekezo na maamuzi**

7.1 Nathibitisha kwamba nimemaliza uchunguzi wangu juu ya mtoto aliyetajwa hapo juu na nina PENDEKEZA/SIPENDEKEZI (Futa inapostahili) kubadilishwa Nyumba ya Kulelea mtoto kama inavyofaa hapo juu.

Saini.....

Jina ..... Tarehe .....

Afisa Ustawi wa Jamii

7.2 Nimethibitisha/Sijathibitisha (futa inapofaa)

Saini..... Tarehe .....

Jina ..... Cheo .....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

(TANGAZO NA ..... LA 2011)

### TAARIFA YA KUKUBALIWA

#### **1. Maelezo ya Nyumba**

1.1 Jina la Nyumba:..... Namba ya leseni:.....

#### **2. Maelezo ya Mtoto**

2.1 **Jina la Kwanza**                   **Jina la Katikati**                   **Jina la Mwisho**

.....   .....                                     .....

2.2 Tarehe ya kuzaliwa ..... 2.3 Jinsia .....

2.4 Mkoa ..... 2.5 Kabilia .....

2.6 Mahali pa kuzaliwa (Inajumuisha wilaya, kata, hospitali)

Maelezo mengine (Hospitali n.k)

.....

#### **3. Matayarisho ya utunzaji kabla ya kumchukua mtoto**

3.1 Hali ya sasa ya mzazi wa mtoto?

Baba: ANAISHI/AMEKUFA/HAJULIKANI (HAONEKANI)

Mama: ANAISHI/AMEKUFA/HAJULIKANI (HAONEKANI)

3.2 Mzazi ameolewa kwa sasa?

.....

3.3 Matayarisho ya kumtunza mtoto kabla ya kumchukua?

.....

.....

#### **4. Maelezo ya Baba**

3.4 Baba wa mtoto anaishi au amekufa ANAISHI/AMEKUFA/HAJULIKANI  
(HAONEKANI)

3.5 **Jina la Kwanza**                   **Jina la Katikati**                   **Jina la Mwisho**

.....   .....                                     .....

3.6 Tarehe ya kuzaliwa                   3.7                           Kabilia .....

.....

3.8 Mahali/Anwani (Ikijumuisha wilaya na kata):

.....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

### **4. Maelezo ya Mama**

4.1 Mama wa mtoto anaishi au amekufa ANAISHI/AMEKUFA/HAJULIKANI  
(HAONEKANI)

4.2 **Jina la Kwanza**      **Jina la Katikati**      **Jina la Mwisho**

..... .....

4.3 Tarehe ya kuzaliwa      4.4 Kabila .....

..... .....

4.5 Anwani yake kwa sasa (Ikijumuisha wilaya na kata):

..... .....

..... .....

### **5. Maelezo ya Ndugu au mlezi (Pale inapohitajika)**

**Jina la Kwanza**      **Jina la Katikati**      **Jina la Mwisho**

..... .....

5.2 Jinsia ..... 5.3 Tarehe ya kuzaliwa ..... 5.4 Kabila .....

5.5 Anwani ya sasa (Ikijumuisha wilaya na kata):

..... .....

..... .....

### **6. Mahitaji ya mtoto**

6.1 Mahitaji ya elimu kwa mtoto (kiwango chake cha elimu kwa sasa)

6.2 Mahitaji maalumu ya mtoto (ikijumuisha ulemavu, magonjwa sugu n.k)

..... .....

..... .....

7. Maelezo ya mapokeo/aliyekubaliwa

..... .....

7.1 Tarehe ya kupokelewa .....

7.2 Sababu ya kupokelewa .....

Saini ..... Tarehe .....

Jina ..... Cheo .....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

C.H. Form No. 2(c)

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO

(GN.NO ...YA 2011)

MAOMBI YA LESENI (MAPENDEKEZO NA UAMUZI)

*Imetungwa chini ya kanuni ZA 5(8),6(1)na 6(2)*

5.Mapendekezo ya Afisa wa ustawi wa jamii

5.1Mapendekezo ya Afisa ustawi wa jamii                   **ANAKUBALI/HAKUBALI**(*futa inapotakiwa*)

Uwezo wa kuchukua watoto:

Umri wa miaka 0-6

Umri wa miaka 7-17

Sababu/masharti

.....

5.2 sahihi ya Afisa Ustawi wa Jamii:

.....

5.3Jina la Afisa wa Ustawi wa Jamii:

.....

5.4 Tarehe.....

### **6 uamuzi**

6.1Uamuzi wa maombi                   AMEKUBALI/AMEKATAA(*futa inapotakiwa*)

Sababu/masharti:.....

.....

*Kanuni za Makao ya Watoto*

---

6.2 Namba ya leseni(kama mwombaji amekubaliwa)

.....

6.3 Sahihi ya Kamishina wa Ustawi wa Jamii ..... Tarehe.....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

C.H. Form No. 3

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO

(GN.NO ...YA 2011)

LESENI YA MAKAO

*Imetungwa chini ya kanuni ya 6(3)(b)*

Hii ni kuthibitisha kwamba:.....(jina la mwombaji)

Ameomba leseni ya kuondesha Mako ya Watoto baada ya kugundua,baada ya uchunguzi,amekidhi vigezo viliwyowekwa chini ya Sheria ya Mtoto na Kanuni zilizotengenezwa chini yake,na ameruhusiwa kuondesha Makazi ya watoto katika

Wilaya: ..... kata.....

Na Makao hayo ya watoto yatajulikana kama:

.....  
Na yatakuwa na uwezo wa kuwa na watoto  
.....

Umri 0-6

umri 7-17

.....  
Kwa leseni Namba:  
.....

Imetolewa na :

Kusainiwa na:

.....  
Kamishina wa ustawi Jamii

Mahali ..... tarehe.....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

C.H. Form No. 4

SHERIA YA MTOTO

## KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO

(GN.NO ...YA 2011)

## RIPOTI YA FEDHA YA MWAKA

*Imetungwa chini ya kanuni ya 15(1)(b)*

1. Numba ya leseni.....
  2. Jina la Makao.....
  3. Anwani.....
  4. Jina la mwenye leseni.....
  5. Jina la meneja.....
  6. Ripoti ya risiti na matumizi ya risisti.....shs ..... matumizi.....shs. Cts
  7. **MICHANGO**

## 7. MICHANGO

# **Fedha taslimu mali**

- a. Serikali ya mitaa
  - b. wazazi
  - c. Watoto
  - d. misaada ya watu
  - e. nje ya michango

## GHARAMA KWA MTOTO MMOJA

8. Makadirio ya ghamama za mtoto kwa siku .....:

WAFANYAKAZI

- ## 9. Wafanyakazi wa Makao.....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

10. Idadi ya wafanyakazi wa ustawi wa jamii.....
11. Namba ya wafanyakazi wa kulea watoto.....
12. Namba ya watoaji.....
13. Idadi ya wafanyakazi(wafagiaji,walinzi).....
14. Una wafanyakazi wangapi walionyeshwa kwenye swalii la 10
  - a. mafunzo ya utabibu au unesi
  - b. huduma ya kwanza
  - c. mafunzo ya jinsi ya kutumia vifaa vya kuzimia moto
  - d. wajibu nje ya makao(cliniki,zahanati n.k)

Sani ya mwenye leseni ..... tarehe.....

Maelezo ya vigezo

+risiti ya zawadi au chakula,nguo,vifaa au michango ambayo imetokana na vitu na sio fedha

\*misaada ya watu binafsi inayopokelewa kutoka sekta binafsi au taasisi ndani ya Tanzania

^ misaada nje ya wafadhili ni misaada nayotoka kwa watu au taasisi nje ya Tanzania

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

C.H. Form NO.5

SHERIA YA MTOTO

KANUNI YA MAKAO YA WATOTO,2011

(TANGAZO NO....LA 2011)

KIBALI CHA KUBADILISHWA KWENYE NYUMBA YA WATOTO

(Kanuni ya 16(2))

Kuhusu suala la.....(Jina la mtoto)

Aliyezaliwa .....tarehe.....

*(nakala ya cheti cha kuzaliwa kinawezza kuhitajika)*

Mimi/sisi tukiwa kama BABA/MAMA/MLEZI (futa inapohitajika) wa mtoto aliyetajwa hapo juu na kutokana na kushindwa kutoa matunzo ya mtoto kwenye familia yetu,tumakubaliana kumleta mtoto aliyetajwa hapo juu kwenye makao ya watoto ambayo imepewa leseni na Kamishna wa ustawi wa jamii.

| Mzazi/mlezi(1)         | Mzazi /mlezi (2)       |
|------------------------|------------------------|
| Sahihi.....            | Sahihi.....            |
| Jina.....              | Jina.....              |
| Uhusiano na mtoto      | Uhusiano na mtoto      |
| <b>Imeshuhudiwa na</b> | <b>Imeshuhudiwa na</b> |
| Sahihi ya shahidi      | Sahihi ya shahidi      |
| Jina la shahidi        | Jina la shahidi        |
| Tarehe                 | Tarehe                 |

**KIBALI CHA AFISA WA USTAWI WA JAMII KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 18  
AU KIFUNGU CHA 137(1) CHA KUBADILISHA MAKAO**

Jina la Afisa wa Ustawi wa Jamii:

Tarehe:

.....  
Sani ya Afisa wa Ustawi wa Jamii:.....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

C.H. Form NO.6

SHERIA YA MTOTO

KANUNI YA MAKAO YA WATOTO,2011

(TANGAZO NO....LA 2011)

**REPOTI YA UCHUNGUZI YA USTAWI WA JAMII**

(KANUNI YA 16(5))

1. Maelezo ya Mtoto

1.1 **Jina la kwanza** ..... **jina la kati kati** ..... **jina la mwisho** .....

1.2 Tarehe ya kuzaliwa.....  
1.3 Jinsia.....  
1.4 Dini.....  
1.5 Kabilia.....  
1.6 Sehemu ya makazi ya sasa.....

2. **Chanzo cha taarifa**

Kutaja vyanzo vyote vya taarifa vinavyotumika kufanya tathimini na ,kama ni muhimu,tarehe:

2.1 Maelezo ya mtoto.....(tarehe)  
2.2. Maelezo ya mzazi/mlezi wamtoto.....(tarehe)  
(eleza ni yupi)

3. **Chanzo cha taarifa**

2.3 Maelezo/kikao na Polisi.....(tarehe)  
2.4 Maelezo/kikao na Afisa afya.....(tarehe)  
2.5 Maelezo/kikao na makao ya watoto.....(tarehe)  
2.6. Mengine(toa maelezo).....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

### **4. Familia iliyopo sasa/hali ya uangalizi**

#### **3.1 Hali ikoje ya wazazi wa mtoto?**

Baba:.....ANAISHI/AMEKUFA(HAYUPO)

Mama .....ANAISHI/AMEKUFA(HAYUPO)

3.2 Hali ya ndoa ya wazazi ikoje?.....

3.3 maandalizi ya uangalizi wa mtoto yakoje?.....

#### **5. Mahitaji ya Mtoto**

4.1 Mtoto anahudhuria shule/mafunzo kwa sasa?.....**ndio/hapana**

(kama ndio(andika aina ya shule/daraja).....

4.2 Mtoto ana mahitaji yoyote maalum ya elimu?.....

4.3 Mtoto ana ulemavu,magonjwa sugu au hali ambayo inahitaji uangalizi maalum?

#### **NDIO/HAPANA**

Kama **Ndio**,toa maelezo.....

### **6. Kuunganishwa na familia**

5.1 Je Mtoto ametelekezwa na wazazi wake? Ndio /hapana

Kama ndio,kwa muda gani?.....

5.2 Jitihada gani zimefanywa kumtafuta mzazi /kumuunganisha mtoto?.....

5.3. Nini Maoni yako juu ya kwa umuhimu wa kuunganisha familia?.....

### **6. Tathmini ya makao ya mtoto**

6.1 Nini maoni yako juu ya umuhimu wa kumweka mtoto katika makao ya watoto?

.....  
6.2 Umeweza kutambua umuhimu wa uwepo wa makao ya watoto? **Ndio/hapana**

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

Kama Ndio, toa maelzoo(kila makao ya watoto yanatakiwa yawe na leseni na kuingizwa katika Taftari-kwa kujaza Fomu maalum(1a au b) and assessment na uamuzi wa Fomu (1c) kwa madhumuni haya)

Jina la Nyumba..... Namba ya  
leseni.....

6.3 Kwanini unaamini kuwa makao ya watoto yanayopendekezwa yanafaa kwa mtoto?.....

6.4 Maoni yako ni nini kwa mtoto?

.....  
.....  
.....

6.5 Nini maoni yako ya umuhimu wa makao ya watoto?.....  
.....  
.....

6.6 Kuna msaada wowote unahitajika kwa ajili ya kumuweza mtoto huyu? **NDIO/HAPANA**

Kama **Ndio**, toa maelezo.....

6.7 Hatua gani ichukuliwe kupata suluhisho la muda mrefu kwa ajili ya huyu mtoto?

.....  
.....

### **7. Mapendekezo & Maamuzi**

**7.1** Thibitisha kwamba umefanya uchunguzi wa jina la mtoto aliyetajwa na kwamba **NINAPENDEKEZA/SI PENDEKEZI** (kata inapotakiwa) kumweka katika Makao ya watoto kama ilivyoelezewa hapo juu.

**Sani:**

.....

**Jina:**..... **Tarehe:**.....

**Afisa ustawi wa jamii**.....

**7.2** Nina **thibitisha/si thibitishi(kata inapotakiwa)** kumweka katika Makao ya watoto kama ilivyoelezewa hapo juu.

Sani.....

Tarehe.....

Jina.....

Kazi.....

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

C.H. Form NO.7

SHERIA YA MTOTO

KANUNI YA MAKAO YA WATOTO,2011

(TANGAZO NO....LA 2011)

RIPOTI YA KUJIUNGA

(KANUNI YA 16(6))

## 1. Maelezo ya Makao

Jina la Makao

**1.1..... Namba ya leseni.....**

## **2. Maelezo ya Mtoto**

**2.1 Jina la kwanza** **jina la kati kati** **jina la mwisho**

.....  
.....  
.....

2.2 Tarehe ya kuzaliwa.....  
2.3 Jinsia.....  
2.4 Dini ..  
2.5 Kabilia.....  
2.6 Sehemu ya kuzaliwa( ikiumuisha Wilaya ,kata na Hospitali )

## **Wilaya Kata**

## Maelezo mengine(Hospital n.k)

#### **4. Maandalizi ya malezi kabla ya kupokelewa**

### **3.1 Hali ya sasa ya wazazi wa mtoto?**

Baba: ..... ANAISHI/AMEKUFA(HAYUPO)

Mama ..... ANAISHI/AMEKUFA(HAYUPO)

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

3.2 Hali ya ndoa ya wazazi kwa sasa?.....

3.3 maandalizi ya mtoto kabla ya kukubaliwa?.....

### **4. Maelezo ya Baba**

3.4 Baba wa mtoto anaishi au  
amekufa?.....**ANAISSI/AMEKUFA/HAJULIKANI (AMEPOTEA)**

3.5 **Jina la kwanza**                           **jina la kati kati**                           **jina la mwisho**

.....

3.6 Tarehe ya kuzaliwa.....

3.7 Kabilia.....

3.8 Anwani ya sasa ikijumuisha (wilaya & kata)

.....

### **4. Maelezo ya Mama**

4.1 Mama wa mtoto anaishi au  
amekufa?.....**ANAISSI/AMEKUFA/HAJULIKANI (AMEPOTEA)**

4.2 **Jina la kwanza**                           **jina la kati kati**                           **jina la mwisho**

.....

4.3Tarehe ya kuzaliwa.....

4.4Kabilia.....

4.5 Anwani ya sasa ikijumuisha (wilaya & kata)

.....

### **5.Maelezo ya MLEZI(kama inahitajika)**

5.1 **Jina la kwanza**                           **jina la kati kati**                           **jina la mwisho**

.....

5.2 Jinsia.....

5.3Tarehe ya kuzaliwa.....

5.4 Kabilia.....

5.6 Anwani ya sasa ikijumuisha (wilaya & kata) .....

**6.Mahitaji ya mtoto**

6.1 Mahitaji ya elimu ya mtoto(mahali alipofikia kwa sasa).....

6.2 Mahitaji yoyote maalum ya mtoto( ikiwemo ulemavu,magojwa sugu,n.k)

.....  
7. Maelezo ya kukubaliwa.....

7.1 Tarehe ya kukualiwa.....

7.2 Sababu za kukubaliwa.....

Saini.....

Tarehe.....

Saini.....

kazi.....

SHERIA YA MTOTO,

KANUNI ZA MAKAO YA WATOTO, 2011

(TANGAZO NO..... LA 2011)

TAARIFA YA MATIBABU

(*Kanuni 18(1)*)

(Ijazwe na Afisa wa Afya)

JIna la Afisa wa Afya aliyefanya uchunguzi .....

Jina la vifaa vyatya afya .....

Tarehe ya uchunguzi wa kitabibu/afya ya mtoto .....

1. Taarifa za msingi

Jina la mtoto .....

Jinsia (K/M) .....

Tarehe ya kuzaliwa .....

Urefu ..... Uzito .....

2. Taarifa za kinga

| Kinga   | Kinga | Tarehe | Kinga       | Tarehe |
|---|-------|--------|-------------|--------|
| Polio   |       |        | Donda koo   |        |
| Ndui  |       |        | Pepopunda   |        |
| Chanjo ya watoto<br>kwa ugonjwa wa<br>kifua kikuu |       |        | Kifua kikuu |        |
| mengineyo   |       |        | Mengineyo   |        |

3. Maelezo binafsi

Mtu anayefanya uchunguzi anasumbuliwa na chochote kati ya haya? Kama ndio onyesha utafiti/matokeo ya utafiti, kama sio, tafadhali andika “HAPANA”

1. Kifua kikuu .....
2. Vidonda vyatya tumbo .....
3. Kutokuwa na mmeng’enjo wa chakula .....
4. Kuharisha .....

5. Homa ya manjano .....
6. Kisukari .....
7. Poliomyletits or other neurological disorders .....
8. Ukoma .....
9. Nervous breakdown .....
10. Ugonjwa wa akili .....
11. Ugonjwa wa macho .....
12. Masikio, pua au ugonjwa wa koo .....
13. Ugonjwa wa ngozi .....
14. Upungufu wa damu .....
15. Magonjwa ya kinamama .....
16. Malaria au magonjwa mengine ya kitropiki .....
17. Kipindupindu .....
18. Kufanyiwa upasuuji .....
19. Ajali .....

Kama jibu lako ni ndio kati ya ugonjwa wowote uliotajwa hapo juu, toa maelezo:

.....  
.....  
.....

4. Uchunguzi wa afya/kitabibu
- 4.1 Afya kwa ujumla  
Afya kwa ujumla .....
- Maambukizi ya ngozi .....
- Meno ..... Koo .....
- Uvimbe unaoongezeka .....
- Macho.....
- Mfumo wa uzazi .....
- Mfumo wa moyo .....
- Utumbo .....
- Mfumo wa fahamu.....
- Ukimwi .....
- 4.2 Uchunguzi
  1. Mkojo .....
  2. Choo .....
  3. Wingi wa damu .....
- 4.3 Matokeo  
Mtoto hana ugonjwa wa kuambukiza .....

*Kanuni za Makao ya Watoto*

---

|  |
|--|
| Ulemavu .....                          |
| Matokeo ya afisa wa afya .....         |
| <b>Maoni ya afisa afya .....</b>       |
| Saini ya afisa wa afya na tarehe ..... |

## *Kanuni za Makao ya Watoto*

---

C.H. Form NO.9

### SHERIA YA MTOTO

### KANUNI YA MAKAO YA WATOTO,2011

(TANGAZO NO....LA 2011)

### KIBALI CHA KURUHUSIWA

### KANUNI YA 23(3)

- Kwa niaba ya .....(jina kamili la mtoto)
- Ambaye yumo katika makazi ya.....(jina la makao ya watoto)
- Mimi.....(jina la afisa wa ustawi wa jamii)
- Ninarhusu kuondolewa kwa mtoto mwenye jina lilitotajwa kwa kutambua kwamba mtoto atakuwa.....  
(ijanzwe pale inapoitajika)
- Jina.....
- Anwani.....
- Mlezi wa kambo.
- Jina.....
- Anwani.....
- ipelekwe kwenye taasisi nyingine
- Jina la makao
- Anwani.....
- Kuruhusiwa baada ya kufikisha miaka 18
- Anwani:.....
- Baada ya kuruhusiwa,nyumba ya watoto haita husika na malezi yoyote ya mtoto.
- Sani ya Afisa Ustawi wa Jamii na Tarehe
- .....

*Kanuni za Makao ya Watoto*

---

C.H. Form NO.10

SHERIA YA MTOTO

KANUNI YA MAKAO YA WATOTO, 2011

(T.S Na....LA mwaka 2011)

TAARIFA YA MWEZI

(*Kanuni ya I8(I)*)

Dar es Salaam,  
27<sup>th</sup> Machi, 2012

HADJI H. MPONDA,  
*Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii*